# Nipashe

Jumanne Juni 22, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580619

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US



Nipashe TESA

Jumanne Juni 22, 2021

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ndizo salamu za wadau shule mchanganyiko

KIPANGA DAUDI NI 'ATLASI' INAYOISHI

Waathirika wanapohoji kulikoni wabakaji wanapewe dhamana

TEKNOLOJIA NA SABATO KASIKA

## Walimu, familia wanavyowapika watoto kuibua vipaji, ubunifu

• Mtoto aunda roboti ya maboksi

**Mahakama** Kuu yatengua uamuzi wa kamati maadili sakata la Fatma Karume

UKURASA 3




**Wakuu** wa mikoa walivyowafunda wakuu wa wilaya

UKURASA 4

UKURASA 11

# Hoja 6 zinazohitaji majibu ya Mwigulu

• **Ni** katika kuhitimisha mjadala wa Bajeti leo... *Endelea ukurasa 2*




## Mdee ashtukia upigaji stempu za kielektroniki

UKURASA 19

## Bilioni 300/- kuwalipa watumishi 70,400 kupandishwa madaraja

UKURASA 3


**MICHEZO** NABI AONYA USAJILI YANGA SC UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan akimwapisha Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Batilda Burian, Ikulu jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Hoja 6 zinazohitaji majibu ya Mwigulu

**Na Waandishi Wetu**

LEO Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, atakuwa na kibarua cha kujibu hoja ngumu sita za wabunge zilizotawala mjadala wa bajeti ya mwaka 2021/22.

Mjadala wa siku saba wa bunge ulitawaliwa na hoja nyingi na kubwa ambazo zilichukua sehemu kubwa ya mjadala ni kodi za laini za simu, kodi ya miamala, ulipaji kodi ya majengo kwa kutumia Luku za umeme na kodi kwenye mafuta.

Nyingine ni upigaji wa fedha kupitia stempu za bidhaa, kupanda kwa leseni na wafanyabiashara wa maduka ya kubadilishia fedha walionyang'anywa fedha zao.

Wabunge walitaka ufafanuzi wa serikali kwenye nyumba za wapangaji, nyumba moja yenye Luku zaidi ya moja na nyumba za udongo zilizoezekwa kwa nyasi zilizopo vijijini.

Aidha, walitaka ufafanuzi wa namna kodi ya miamala ya simu na laini za simu zitakavyotozwa, huku kukiwa na hofu ya wananchi wengi kuumia.

Wengine walipongeza kuwa kuna ubunifu katika kutafuta kodi kwa kuwa sasa kodi ya majengo itapatikana kirahisi kupitia malipo ya umeme.

Mapendekezo ya bajeti hiyo ni kutoza kodi ya simu ya Sh. 10 hadi Sh. 200 kila siku kwa kila mwenye laini ya simu, na iwapo itapita itaanza kutekelezwa Julai mosi, mwaka huu.

Nyingine ni kutoza kodi ya Sh. 10 hadi 10,000 kwa mwezi kwa kila muamala wa simu utakaofanywa na watumiaji.

Aidha, imependekezwa kutozwa kodi ya majengo ya Sh.1,000 kila mwezi kwa nyumba za kawaida na Sh. 5,000 kwa ghorofa.

Baadhi ya wabunge waliochangia hoja hiyo ni pamoja na Mbunge wa Viti Maalum CCM, Juliana Shonza, Mbunge wa Jimbo la Vunjo, Dk. Charles Kimei, Mbunge wa Muleba Kaskazini, Charles Mwijage, Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee na Mbunge wa Same Mashariki, Anne Kilango.

**KODI YA MAJENGO**

Wabunge hao walisema ni vyema serikali ikafafanua kwa kina kodi ya majengo italipwa na nani kwa kuwa zipo nyumba zinakaliwa na wapangaji jambo ambalo huenda wakabeba mzigo mzito.

"Sheria ya majengo ya awali inasema kwamba suala la kulipa kodi ya majengo ni la mwenye nyumba na siyo la mpangaji.

"Kwa hiyo kwenye agizo hili nimwombe sana waziri atakaposimama hapa atuambie serikali imejipangaje, ina mkakati gani ili kuondoa sintofahamu kati ya mwenye nyumba na mpangaji.

"Waziri utuambie kwa wazee wenye msamaha itakuwaje, na kuna zile nyumba ambazo unakuta ni nyumba moja lakini kila mtu ana Luku yake utaratibu uko vipi, pia kuna maeneo ambayo yalikuwa nje ya wigo wa kodi ambayo ilikuwa haiwagusi, je, serikali imejipangaje kuhakikisha wakati wa kuikusanya haileti mgongano?" alisema.

"Waziri ukija hapa ni vizuri ukafafanua kuhusu hii kodi kwa kuwa italeta mikanganyiko kwa wananchi ikiachwa hivi ilivyo," alisema Kilango.

**KADI LAINI ZA SIMU**

Baadhi ya wabunge waliochangia hoja hiyo walitaka fedha zitakazotokana na tozo hizo ziwekwe kwenye mfuko maalum, ili zikatekeleze mambo yaliyokusudiwa badala ya kuingia serikalini na kupangiwa shughuli nyingine.

Mbunge wa Ilala, Mussa Zungu, ambaye aliibua hoja ya kodi hiyo, alisema wanaotoa maneno ya kashfa na matusi dhidi ya viongozi kwenye mitandao ya kijamii kuhusu suala hilo wajue wanalipa kodi kwa kutuma ujumbe huo.

Aidha, Kamati ya Bajeti walisema ubunifu wa kodi ya majengo ni mzuri ila unakwenda kinyume cha sheria ya kodi ya majengo ambayo inaangalia majengo yaliyoko maeneo yanayotakiwa kulipiwa kodi.

"Mapendekezo haya yanachukulia nyumba zote zenye umeme hata zile ambazo ziko vijijini, lakini hazipo kwenye maeneo ambayo kwa mujibu wa sheria hazina sifa ya kutozwa kodi," alisema Sillo Baran.

Pia alisema mapendekezo hayo hayatoi msamaha kwa taasisi za umma na majengo mengine ya umma ambayo yanatumia umeme lakini kwa mujibu wa sheria yamesamehewa.

"Kuweka kiwango hiki kwa nyumba zilizoko mjini na vijijini ni kuwaumiza wananchi ambao wanaishi vijijini. Kamati inashauri ubunifu uende sambamba na tathmini ya nyumba na kutumia Luku kwa namba ya mlipa kodi na kila Luku itozwe kulingana na nyumba ambayo Luku hiyo ipo," alisema.

"Utaratibu uwekwe kwa majengo ya maghorofa ambayo yana mkazi zaidi ya mmoja. Hatua hii italeta mapato zaidi kuliko utaratibu huu unaopendekezwa.

**KODI YA MAFUTA**

Mbunge wa Kaliua, Aloyce Kwezi na Mbunge wa Viti Maalum, Neema Lugangila, walipendekeza kampuni za simu kuchangia kiasi kiasi cha Sh.1,000 kwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kwa sababu barabara za vijijini ndiyo mishipa ya uchumi.

Baadhi ya wabunge walisema hoja siyo tozo hizo bali ni mzigo utakaokuwa unabebwa na kila lita ya mafuta na kuchangia mfumuko wa bei sekta ya usafirishaji na bidhaa.

Pia walishauri kiwango cha Sh. 100 iliyotengwa kwenye mafuta kwa ajili ya TARURA ipelekwe kwa wakati badala ya fedha hizo kupelekwa miezi sita au mwaka au siku za mwisho za kumalizia bajeti.

Mbunge wa Muleba Kaskazini (CCM), Charles Mwijage na Mbunge wa Jimbo la Ndanda (CCM), Cecil Mwambe, walisema kuwa barabara hizo zinatumia fedha nyingi za wananchi na nyingi hazipitiki na nyingine zimekosa mifereji.

Walitaka kufahamu fedha iliyokusanywa kwa ajili ya miradi ya barabara na maji kwa awamu iliyopita mpaka sasa imekwenda kiasi gani na chenji iliyobaki itapatikana lini.

**MADUKA YA KUBADILISHIA FEDHA**

Mbunge wa Arusha Mjini, Gambo, alitaka ufafanuzi wa fedha zilizochukuliwa kwenye maduka ya kubadilishia fedha, magari, hati za vyumba na viwanja vya wafanyabiashara jijini Arusha pamoja na kupanda kwa leseni ya duka hilo kutoka Sh. milioni 300 hadi bilioni moja.

**UPIGAJI**

Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee, aliitaka serikali kuja na majibu ni lini itavunja mkataba wa uwekaji wa stempu za kielektroniki kwenye bidhaa mbalimbali, kati yake na Kampuni ya Societe Industrielle de Produits Alimentaire (SICPA) ya Uswisi, yenye ubia na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

## 'House girl' adaiwa kumnyonga mtoto wa bosi

**Na Tumaini Mafie, ARUSHA**

MSICHANA wa kazi za nyumbani mkazi wa Olasiti mkoani Arusha (jina limehifadhiwa), anadaiwa kumnyonga hadi kufa mtoto wa tajiri yake mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, alisema kuwa tukio hilo lilitokea Juni 19, mwaka huu majira ya saa 12 jioni.

Alisema mtoto huyo aliyefahamika kwa jina la Tifani Osward anadaiwa kuuawa kwa kunyongwa shingoni hadi kufariki na msaidizi wa kazi za nyumbani, ambaye jina lake limehifadhiwa kwa sasa.

"Msichana huyu aliachwa nyumbani na mtoto, huku taarifa za awali zinaonyesha kuwa aliajiriwa miezi miwili iliyopita na bosi wake huyo akitokea mkoani Mara," alifafanua Kamanda.

Aidha, alisema mtuhumiwa huyo anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa upelelezi zaidi ili kubaini chanzo cha tukio hilo, na kwamba upelelezi utakapokamilika jalada litafikishwa kwa Mwendesha Mashtaka wa Serikali kwa hatua zaidi.

"Nitoe wito kwa wazazi na walezi kufuatilia mienendo ya wasaidizi wao wa ndani kabla na baada ya kuwaajiri, ili kufahamu tabia zao vizuri na pia kuweza kuwaamini wanapokuwa wamewaachia familia na majukumu ya nyumba," alisisitiza kamanda huyo.

## Kamati Kuu CCM kukutana leo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), leo inatarajiwa kukutana chini ya Mwenyekiti wake Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan, jijini Dodoma.

Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi wa chama hicho, Shaka Hamdu Shaka, kupitia taarifa yake aliyoitoa jana, alisema kikao hicho ni cha kawaida.

"Ni kweli Juni 22 (leo) Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, ataongoza kikao cha kawaida cha kamati kuu, maandalizi yote yamekamilika, ni kikao cha kawaida cha kikatiba," alisema Shaka.

Alisema kikao hicho kimetanguliwa na Kikao cha Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, kilichofanyika chini ya Mwenyekiti wake Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo.

Kikao hicho kinakutana huku baadhi ya wajumbe wake wakiwa wameteuliwa kwenye nyadhifa mbalimbali serikalini.

HABARI KITAIFA

# Korti yatengua uamuzi sakata la Fatma Karume

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania imetengua uamuzi wa Kamati ya Maadili ya Mawakili iliyomfutia uwakili, Fatma Karume, na kuamuru malalamiko yapelekwe katika Kamati ya Mawakili.

Uamuzi huo ulitolewa jana mbele ya jopo la majaji watatu lililoongozwa na Jaji Issa Maige, baada ya mawakili wanaomtetea Fatma, Peter Kibatala na Dk. Rugemeleza Nshalla kupinga uamuzi uliotolewa na Kamati ya Maadili baada ya Jaji Kiongozi, Eliezer Feleshi, mwaka 2019 kuelekeza shauri hilo likasikilizwe na kamati hiyo.

Jopo hilo baada ya kupitia hoja mbalimbali zilizowasilishwa lilitengua adhabu ya kufutiwa uwakili na kutoa amri kwa ajili ya utekelezaji.

Malalamiko yaliyosababisha kufutwa kwa uwakili yaliwasilishwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kesi ya Ado Shaibu.

Mahakama katika uamuzi wake iliamuru kwamba malalamiko yapelekwe katika Kamati ya Mawakili ndio watakaotoa uamuzi dhidi ya Fatma.

"Kwa uamuzi huo Fatma atakuwa na nafasi ya kujitetea, amerudishiwa uwakili wake, hivyo anayo haki ya kujitetea," alisema Dk. Rugemeleza Nshalla.

Pia Mahakama Kuu imeamuru Msajili wa Mahakama hiyo ndio apeleke malalamiko yaliyowasilishwa na AG kwa Jaji Kiongozi katika kesi ya Ado Shaibu, Katibu wa Uenezi wa Chama cha ACT-Wazalendo aliyekuwa akipinga uteuzi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali(AG).

Akizungumzia hilo Wakili Peter Kibatala alisema mwenendo wote wa kamati ya maadili ya mawakili umeamuliwa na Mahakama hiyo ufutwe na kwamba hoja zao za kupinga kufutwa kwa Fatma zilikuwa 13.

Awali, Mahakama Kuu baada ya kupokea malalamiko iliamuru Fatma apelekwe kamati ya maadili kwa madai ya kushambulia ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Karume alisimamishwa kazi huku sababu yake ikitajwa kuwa kile alichokizungumza katika kesi iliyofunguliwa na Ado.

Mawakili wa Serikali walilalamikia maneno yalioandikwa na Fatma wakati walipokuwa wakifungua kesi hiyo Mahakama Kuu.

"Hata iwapo kesi hii itashindwa ataendelea kupambana nayo, rais akiondoka madarakani mwaka 2020 au kama ataondoka 2025 au kama mahakama itabadilika ataendelea kupambana."

Katika ukurasa wake wa Twitter, Fatma aliwashukuru mawakili hao kwa kuandika "Ninataka kuwashukuru Kibatala, Nshala, Prof. Issa Shivji, Mike Ngalo na wote mlionisimamia kesi yangu mbele ya jopo la Majaji wa Mahakama Kuu."

"Jopo la Majaji Mahakama Kuu limechukua chini ya miezi tisa maamuzi ya kusema maamuzi ya Advocate's Committee (kamati ya mawakili) ni haramu. Kwa hilo nashukuru," alisema.



Aliyekuwa Katibu Tawala mkoani Tanga, Judica Omari (kulia), akikabidhi ofisi kwa Katibu Tawala mpya, Pili Mnyema (kushoto), katikati ni Mkuu wa Mkoa, Adam Malima. Judica ameteuliwa kuwa Katibu Tawala mkoani Njombe. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA.**

# Bil. 300/- kuwalipa waliopanda madaraja

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imesema hadi jana asubuhi watumishi wa umma 70,437 kati ya 91,841 wamepandishwa, huku Sh. bilioni 300 tayari zimetolewa kuwalipa.

Aidha, Sh. bilioni 23 zimetolewa kulipa malimbikizo kwa watumishi 11,983 ikiwamo walimu.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Mohamed Mchengerwa, alibainisha hayo jana alipokuwa kwenye kikao kazi cha Wakuu wa Idara za Utawala na Rasimali Watu katika utumishi wa umma. Alisema taratibu zote za upandishaji zinaendelea na watumishi hao waliopanda vyeo watapata mishahara ya mwezi huu kulingana na madaraja yao waliyopandishwa.

Aidha, alisema serikali imetoa fedha za kulipa malimbikizo ya watumishi hao, ambayo yatalipwa mwisho wa mwezi huu.

"Rais Samia ameshatoa kibali cha kupandisha madaraja watumishi 91,841 hivyo watumishi wote wenye sifa ya kupandishwa madaraja watapandishwa na kupewa haki yao," alisema.

Waziri Mchengerwa aliwataka maofisa hao kutimiza wajibu wao kwa kutenda haki kwa watumishi na wananchi.

"Kuna baadhi ya watumishi taarifa zao ninazo, walevi kupindukia, hiyo inasababisha kutofanya kazi kwa weledi maana mara nyingi muda hutumia katika ulevi," alisema.

Alihimiza michango ya watumishi ipelekwe PSSSF haraka ili wastaafu wapate mafao yao kwa wakati.

Waziri huyo alisema mtumishi yeyote atakayezembea katika kitengo chake atachukuliwa hatua haraka ikiwamo kumwondoa katika nafasi aliyopo.

Mchengerwa alisema kuwa hatawavumilia watumishi wala rushwa, wabadhirifu wa mali za umma na watakaotoa siri za serikali nje watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Alionya taasisi yoyote kutotengeneza mfumo wa malipo ya serikali bila kufuata sheria za taratibu za sheria ya mtandao ya serikali.

"Tukigundua kuna mtu au taasisi yoyote ya serikali imetengeneza mfumo wa malipo bila kufuata taratibu na sheria za serikali za mtandao kama yuko chini ya wizara yangu nitamwondoa kazini, kama hayupo chini yangu nitafuata taratibu za kumwondoa," alisema.

# Luku za maji kuanza rasmi mwaka huu

**Na Mwandishi Wetu**, DODOMA

SERIKALI imesema kuanzia Julai mwaka huu, mfumo wa mita za malipo kabla ya matumizi kwa wateja wa maji utaanza ili kuondoa malalamiko ya wananchi kubambikiwa ankara za maji.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua kikao cha ushirikiano baina ya Wizara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) zenye dhamana ya sekta ya maji.

Alisema anategemea ndani ya wiki mbili zijazo maandalizi yatakuwa yamekamilika na wateja wataanza kufungiwa rasmi kuanzia Julai, mwaka huu.

"Kwa sasa kuna malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu kubambikiziwa ankara za maji, mfumo huu wa kufunga mita za Luku, kabla ya matumizi yake tujue umependwa na watu wengi kwa sababu mteja atalipa kwanza halafu ndio anapata huduma," alisema.

Alisisitiza SMT na SMZ kuanza kutenga maeneo kwa ajili ya kuhifadhi majitaka ambapo kwa sasa ni asilimia 30 ya maji taka ndio yanayohifadhiwa.

"Itakuwa haina maana yoyote kama nguvu kubwa kuwekwa katika majisafi halafu wakasahau namna ya kuhifadhi majitaka, kwani utafiti unaonyesha kuwa ukipeleka maji asilimia 80 kati ya hizo 40 yatakuwa majitaka," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini Zanzibar, Dk. Mngereza Mzee Miraji, alisema wizara hiyo imepokea ushirikiano wa kisekta na Tanzania Bara.






Wahifadhi wastaafu na watumishi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), wakiwa eneo la ushoroba, walipokuwa wakifanya utalii wa ndani katika Msitu wa Asili wa Pugu Kazimzumbwi, Kisarawe mkoani Pwani juzi, ikiwa ni hafla ya kuwaaga wastaafu 79 wa wakala huo.PICHA: JUMANNE JUMA

# Wakuu wa mikoa wawafunda Ma-DC

**Na Waandishi Wetu**

WAKUU wa wilaya wapya wamepewa majukumu mazito wanayopaswa kuyatekeleza, ikiwamo kwenda kutatua migogoro ya ardhi, kupanua sekta ya kilimo, kutenga maeneo kwa ajili ya wamachinga pamoja na kutokomeza vitendo vya uhalifu.

Mbali na hilo, wametakiwa kutotumia vibaya madaraka yao kwa kuweka watu ndani, kwenda kusimamia vizuri mgawanyo wa mashamba pori yaliyofutwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

**MOROGORO**

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, aliwataka wateule hao katika wilaya tano za mkoa huo kwenda kusimamia mgawanyo wa mashamba yaliyofutwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema wakuu hao hawana budi kusimamia mgawanyo huo na kuhakikisha wanaopata maeneo wanajulikana na utaratibu wa kupata maeneo unajulikana mapema ili kuepusha malalamiko.

Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando, alitaja vipaumbele vyake kuwa ni pamoja na kutatua kero za wananchi ikiwamo migogoro ya wakulima na wafugaji, ndoa, mirathi.

Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Hanji Godigodi, aliahidi kuwaelimisha wananchi wa wilaya hiyo na wilaya jirani waliovamia Bonde la Mto Kilombero kwa kilimo na ufugaji juu ya umuhimu wa eneo hilo linalopeleka maji kwenye Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere.

**PWANI**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, aliwaagiza wakuu wa wilaya wateule kwenda kusimamia sheria katika utatuzi wa migogoro ya ardhi.

Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri alisema ataanza kwa kukaa na wananchi kwenye maeneo ya migogoro kuitafutia ufumbuzi.

Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Nickson Saimon, alisema pamoja na nafasi aliyopewa mchango wake katika sanaa utaendelea kuwapo katika ajenda za kitaifa, mkoa na wilaya.

**ARUSHA**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, aliwataka wakuu wa wilaya wapya kuacha kuendekeza majungu, badala yake wafanye kazi katika kuleta maendeleo ya mkoa huo.

Mkuu wa wilaya ya Arusha, Sophia Mjema, alisema yupo tayari kuleta maendeleo na mabadiliko makubwa, kwani Arusha ni Jiji la utalii, hivyo ataendeleza yale aliyotoka nayo katika uongozi kwa kipindi cha miaka 15 na aliomba ushirikiano zaidi katika maendeleo. Naye Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Raymond Mangwala, alishukuru Rais Samia kwa kumchagua na aliahidi kuleta maendeleo.

**TANGA**

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima, aliwataka wakuu wa wilaya wateule kuhakikisha sekta ya kilimo kwenye maeneo yao inakuwa na tija kwa kuleta matokeo chanya ya ongezeko la uzalishaji, uhakika wa soko pamoja na kukuza pato la mkulima na kuimarisha uchumi wa mkoa.

Kadhalika, aliwataka viongozi hao kutotumia mamlaka yao vibaya ikiwamo kufanya vitendo ambavyo ni kunyume na maadili ya utumishi wa umma ikiwamo kuweka watu ndani,kutumia lugha chafu na za kuudhi, ulevi na badala yake wajikite katika kufuata kanuni,taratibu na sheria za kazi.

Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Basila Mwanukuzi, alisema miongoni mwa vipaumbele anavyoenda kutekeleza ni kuhakikisha yale yote yaliyoainishwa katika ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, Kalisti Lazaro, alisema mbinu alizotumia katika kuimarisha sekta ya elimu wakati akiwa Meya wa Jiji la Arusha ndiyo atakazotumia akiwa wilayani humo lengo kuu ni kuhakikisha kwamba wilaya hiyo inaongoza katika matokeo ya mitihani kwa ngazi zote.

**SHINYANGA**

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, aliwataka wakuu hao wa wilaya kwenda kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za kazi, pamoja na kutatua changamoto za wananchi bila ya kuchoka.

Aidha, aliwataka wakuu hao kwenda kusimamia halmashauri na kubuni vyanzo vipya ya mapato, pamoja na kuifanya bandari ya Isaka iwe kituo kikubwa cha biashara.

Mkuu Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alisema jukumu lao ni kutumikia wananchi na kuwaletea maendeleo, jambo ambalo aliahidi kulifanyia kazi.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, aliawahidi wananchi wa wilaya hiyo kuwaletea maendeleo, pamoja na kutunza mazingira.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, aliahidi kuendeleza yale ambayo aliyaanzisha kwa ajili ya kutumikia wananchi na kuwaletea maendeleo.

**MWANZA**

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, aliwataka wakuu hao kwenda kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda ili kuleta mageuzi katika sekta hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, alisema ajenda yake ya kwanza itakuwa ni suala la ulinzi na usalama kwa eneo hilo kuwavutia wawekezaji.

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, aliahidi kushirikiana na jamii ili kutatua kero mbalimbali zinazowakabili.

Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kalli, aliahidi kufuatilia fedha za maendeleo kwa kila sekta ikiwemo afya, elimu, maji na barabara ili zifanye kazi kama ilivyoelekezwa katika miradi ya maendeleo.

Mkuu wa Wilaya ya Kwimba, Johari Samizi, alisema suala la usalama na utulivu ni suala muhimu kwa jamii yoyote na kwamba atafanya hivyo ili kuleta maendeleo.

**IRINGA**

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, aliwataka wakuu wa wilaya wateule kwenda kufanya kazi kwa bidii na siyo kujifungia barabarani. Aliwataka kwenda kusimamia ukusanyaji wa mapato na miradi ya maendeleo.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Muhamed Hassan Moyo alisema kipaumbele kikubwa atakachoanza nacho ni kuhakikisha ulinzi na usalama wa Mkoa wa Iringa unaimalika kwa kiwango kikubwa.

Mkuu wa Wilaya Mufindi, Saad Mtambule alisema kuwa kipaumbele chake kikubwa ni kuhakikisha anaenda kushughulikia migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ni kero kibwa kwa wananchi.

Imeandaliwa na Zuhura Zukheir (Iringa), Neema Emmanuel (Mwanza), Marco Maduhu (Shinyanga), Lulu George na Boniphace Gideon (Tanga), Cynthia Mwilolezi (Arusha), Julieth Mkireri (Pwani), Christina Haule (Morogoro).

# Mtaji wa maduka ya fedha moto bungeni

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

TAKWA la kisheria linalotaka kila mfanyabiashara anayetaka kuomba kufungua tena biashara ya maduka ya kubadilishia fedha, maarufu Bureau De Change, kuwa na mtaji wa Sh. bilioni moja, badala ya Sh. milioni 300, limelitikisa Bungeni.

Wabunge wamedai kiwango hicho cha mtaji wa Sh.bilioni moja kilichowekwa ni mzigo na serikali inachopaswa kukifanya ni kutazama upya kiwango hicho na kufanya marekebisho.

Akichangia jana mjadala kuhusu hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2020 na mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na makadirio ya mapato na manunuzi ya serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22, Mbunge wa Gando, Zanzibar, Mussa Omari Salim, alisema:

"Mheshimiwa Naibu Spika (Dk. Tulia Ackson), haiingi akilini mwangu hata kidogo, uwe na Sh. milioni 300 (sasa shilingi bilioni moja) mtaji wa kufungua Bureau De Change. Binafsi kabisa, naiomba serikali kupitia Wizara ya Fedha iliangalie tena jambo hili.

"Wafanyabiashara wengi waliopo Dar es Salaam, ni wapigakura wetu au ni ndugu wa wapigakura wetu.

Sisi kutokea Pemba, tumejikita sana katika biashara, unapofunga moja kati ya component za biashara (sehemu ya biashara) unatuua kiuchumi. Unapoweka kizingiti katika biashara kama ya Bureau De Change, unaua kabisa.

"Mheshimiwa Naibu Spika haiingi akilini mwangu hata kidogo uwe na Sh. milioni 300 mtaji wa kufungua Bureau De Change, binafsi kabisa naiomba serikali kupitia Wizara ya Fedha iliangalie tena jambo hili."

Wakati anachangia kuhusu maduka hayo, Mbunge wa Iringa Mjini (CCM), Jesca Msambatavangu, alisimama na kumpa taarifa Mussa Omari Salim, akisema requirement (mahitaji ya lazima) ya kuanzisha Bureau De Change kutokana na kanuni mpya ya Mwaka 2019, ni Sh. bilioni moja na sio milioni 300 kama anavyosema, hiyo ilifutwa.

Baada ya kupewa taarifa hiyo, Mbunge huyo wa Gando, alisema kiwango hicho cha mtaji wa bilioni moja, kwao Pemba ni kichakaa, tunaita ni balaa.

"Binafsi mimi mpaka namaliza Chuo Kikuu pale JUCC nikichukua Diploma yangu ya Tekonolojia na Mawasiliano, sikuwahi kufikiria kuajiriwa na serikali na huu ubunge haikuwa ndoto yangu, nimekuja tu kwa sababu nilihisi ninao uwezo wa kuwasemea wananchi wa Gando Bungeni.

Nilitegemea sana kujiajiri, lakini kunapokuja vizingiti kama hivi sidhani kama wale ambao hawajabahatika wanaweza kuwa na uwezo wa kujiajiri. Jambo hili niko 'serious' ndani ya Dar es Salaam nikuwa na rafiki zangu ambao walikuwa na Bureau De Change yapata 125.

Leo hii wamekaa 'dormant', lakini sio wao hata wale ambao walikuwa na wafanyakazi wao wamerudi Pemba na ndio hao wameshika mabango kuitukana serikali na wakiambiwa waandamane na wale wasioitakia mema serikali."

HABARI KITAIFA

# Madereva darasani kupunguza ajali

**Na Christina Mwakangale**

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kimeanzisha darasa la kutoa elimu kuhusu usalama barabarani, kwa madereva wa mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani ikiwa ni mkakati wa kupunguza ajali.

Jeshi hilo limesema pamoja na ajali za barabarani kupungua, bado kuna haja ya elimu hiyo hususan kutoa ushauri wa kisaikolojia baada ya kubaini baadhi ya ajali hutokana na msongo wa mawazo wa madereva ambao hawana ajira.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, SACP Wilbroad Mutafungwa, aliyasema hayo jana, kwenye kituo cha mabasi cha Magufuli, Mbezi, mkoani Dar es Salaam, wakati kikosi hicho kikitoa elimu kuhusu usalama barabarani, akisema hiyo elimu imefanikisha kupunguza ajali.

Alisema madarasa yaliyofunguliwa na kikosi hicho kwenye kituo hicho, yatakuwa endelevu na yatatoa elimu kwa madereva wote bure, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwamo Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) na Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI).

Alisema wadau wengine watakaohusishwa ni wamiliki wa mabasi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Shirika la Bima la Taifa (NIC), Mabalozi wa Usalama Barabarani (RSA) pamoja na Chuo cha Usafiri cha Taifa (NIT).

Kamanda Mutafungwa alisema mara kadhaa wakiwahoji baadhi ya madereva na sababu za ajali walizopata, hutaja kunatokana na kutokuwa na utulivu wa kiakili unaosababisha msongo wa mawazo, kutokana na kufanya kazi ambayo si ajira ya kudumu.

"Tunatoa elimu hii kuhusu namna ya kuongeza usalama barabarani, tumeona madereva wengi hupata ajali sababu wana msongo wa mawazo, baada ya akili yao kutokuwa sawa akiwa kazini, kwanza hana uhakika na kazi sababu si ya mkataba wa ajira.

"Baada ya elimu hii dereva akisababisha ajali, tutamchukulia hatua kali za kisheria, kwa sababu elimu tumempatia. Darasa hili la kutoa elimu litakwenda na mikoa mingine, pamoja na kwamba tunafahamu walipata leseni baada ya kujifunza," alisema Kamanda Mutafungwa.

Kadhalika, Kamanda Mutafungwa alisema ushiriki wa wamiliki wa mabasi ili kupokea matatizo yanayowakabili madereva kutokana na kufanya kazi ambayo si ajira na kutatua tatizo hilo.

Mkuu wa Ukaguzi wa Magari Tanzania kutoka Kikosi cha Usalama Barabarani, ASP Ibrahimu Samwix, alisema ukaguzi wa magari kila baada ya kilomita 300, husussani yanayofanya safari ndefu, ikiwamo mabasi yaendayo mikoa na nchi jirani, ni muhimu na husaidia kubaini hitilafu.

Alisema jeshi hilo limebaini kwamba ukaguzi wa magari ya masafa marefu kabla, katikati na baada ya safari huepusha ajali ambazo kwa kiwango kikubwa hutokana na sababu za kibinadamu ikiwamo uzembe.

Bingwa wa Magonjwa ya Ajali na Mifupa kutoka MOI, Dk. Kennedy Nchimbi, alisema taasisi hiyo hupokea takribani majeruhi wa ajali 20, ambao wengi wao huhitaji upasuaji na kuwekewa vyuma.

"Wanaopata ajali huwa wanategemewa, wanapojeruhiwa au hata kufariki ni gharama kubwa katika jamii na serikali kwa sababu uchumi kuanzia familia hadi taifa utazorota," alisema Dk. Nchimbi.

## PSSF, Azania kuuza nyumba mkopo nafuu

**Na Elizabeth Zaya**

MFUKO wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSF) na Benki ya Azania, wameingia makubaliano ya uuzaji wa nyumba na viwanja vya gharama nafuu kwa utaratibu wa mkopo.

Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji wa saini ya makubaliano hayo jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa PSSSF, Hosea Kashimba, alisema lengo la kuingia makubaliano hayo ni kuwawezesha wanachama na wananchi kwa ujumla kumiliki nyumba kwa utaratibu wa kulipa kidogo kidogo.

Alisema mradi huo wa nyumba za gharama nafuu upo katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Shinyanga, Tabora, Mtwara na Iringa.

Mradi wa viwanja hivyo vya bei nafuu alisema upo katika mikoa ya Ruvuma, Kagera, Tabora, Iringa, Katavi, Morogoro, Dar es Salaam, Rukwa, Lindi na Mtwara.

Alisema wananchi watafaidika kwa kukopeshwa nyumba na viwanja kwa riba ndogo ya asilimia 10 kwa mwaka na hivyo kuimarisha na kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kwa kuwa na makazi bora.

Alisema kupitia makubaliano hayo, jumla ya nyumba 192 na viwanja 886 vyenye hati vitakuwa sokoni na vitauzwa kwa njia ya mkopo wenye riba nafuu utakaotolewa kwa wanachama kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Azania, Charles Itembe, alisema nyumba hizo ziko za aina nne na zenye ukubwa tofauti kuanzia za vyumba viwili hadi vinne.

"Bei ya nyumba ni kati ya Sh. milioni 36 hadi Sh. milioni 61 na hii inategemea na ukubwa wa nyumba husika na bei zimejumuisha na kodi ya ongezeko la thamani(VAT)," alisema Itembe.




Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, akibeba mtoto mgongoni kuadhimisha Siku ya Kinababa Duniani iliyowataka wanaume kubeba viatu vya kinamama kuonja adha inayowakumba wakati wa malezi ya familia, huku Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Yasinta Mboneko, akionekana kufurahishwa na hatua hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Siku 7 kwa mrajisi ushirika kurejesha vyama 32 kahawa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amempa siku 7 Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, Dk. Benson Ndiege, kuhakikisha anaurejesha Umoja wa Vyama vya Msingi 32 vya Wakulima wa Kahawa (G32 KNCI JVE) vinavyofanya biashara ya kahawa.

Waziri Mkenda alitoa agizo hilo kufuatia hatua ya mrajisi huyo kuufuta umoja huo Agosti mwaka jana, kwa madai ya kuwa biashara ya kahawa inapaswa kufanywa na Chama cha Ushirika KNCU pekee, jambo ambalo amesema sio sahihi.

Akizungumza juzi katika mkutano wa 11 wa wadau wa kahawa uliofanyika jijini Dodoma ambao uliwakutanisha wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya wakurugenzi, taasisi za fedha pamoja na viongozi mbalimbali wa vyama vya msingi, alisema endapo akishindwa kuurejesha umoja huo, hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwamo kufutwa kazi.

"Kuna watu walikuwa wameungana wanajiita G32, nimempa Mrajisi wiki moja amalizane na hawa watu ili biashara ya kahawa iendelee...kahawa ndio iliyotuletea ushirika wa kwanza hapa Tanzania na KNCU ilizaliwa kutokana na kahawa, na mimi sitaki ife," alisema Prof. Mkenda.

"Ndani ya wiki hiyo moja nataka G32 iwe imeanza kazi, kwa sababu kazi ya ofisi ya Mrajisi inatakiwa iwe facilitative (iwezeshe), maana kuna wengine walikuwa wanazuia kahawa isiende kwenye uchakataji," alisema Prof. Mkenda.

Akizungumza baada ya waziri kutoa agizo hilo, Meneja Mradi wa G32, Gabriel Ulomi, aliishukuru serikali kwa maamuzi hayo, na kusema kuwa ni moja ya hatua ya kuwarejeshea uhai.

"Kwa niaba ya kundi la vyama vya G32 tunashukuru awamu ya sita kusikiliza kilio cha wakulima wa kahawa ambao tumekuwa tukikusanya kahawa kutoka kwa wakulima na kuuza ndani na nje ya nchi kwa kurejeshea haki yetu ya kimsingi ya kufanya biashara kwa sheria za nchi kwa sababu ushirika ni uhai," alisema Ulomi.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## MA-DC kuweni na hofu ya Mungu, acheni kujilewesha madaraka

**HONGERENI** wakuu wa wilaya mlioteuliwa. Kwa wapya mna mengi ya kujifunza na kubwa zaidi ni kuwa na hofu ya Mungu na kuwajali watu mnaowatumikia kwa kuhakikisha kuwa wanapelekewa maendeleo na si vinginevyo.

Pili hakikisheni fedha za miradi ya maendeleo zinafikishwa vijijini badala ya kuliwa na wajanja.

Wakati mnaendelea kutafakari uteuzi na kuangalia majukumu yenu kwa mujibu wa katiba, kumbukeni kuwa Tanzania ni ya kudumu lakini ninyi mnapita. Na kitakachofanya mzidi kukumbukwa na kuheshimiwa ni alama mtakazoacha kutokana na majukumu mtakayoyafanya hasa ya kuinua maisha ya watu kutoka umaskini hadi hali bora.

Uongozi wenye sifa za ujasiriamali ndicho kinachohitajika zama hizi si kukaa ofisini muda wote bila kujiongeza.

Mathalani, kwenye wilaya zenu kuna vitega uchumi ambavyo bado havijaendelezwa mfano, maeneo ya minada ya kuuza mifugo, hamasisheni kuweka miundombinu kama hoteli, masoko na viwanda vidogo vya kisasa ili kuongeza thamani maeneo hayo.

Kuna wilaya ambazo matunda hayakauki kwa maana kuwa kila mwezi yanazalishwa hivyo kuweni wajasiriamali wekeni viwanda vidogo kuzalisha juisi, maghala kuhifadhi matunda au kuweka masoko ya kisasa kuvuta magari yenye wateja wanaoweza kusimama maeneo hayo na kununua bidhaa.

Wakati mwingine tunaona kuwa yapo maelekezo kuwa kila basi liingie kwenye stendi kuu ya wilaya na kuacha tozo kwa ajili ya Wakala wa Barabara wa Taifa (TANROADS) na ule wa Barabara za Ndogo za Mijini na za Vijijini (TARURA), mnaweza kuweka utaratibu pia mabasi hayo yakaagizwa kusimama kwenye masoko bora mnayojenga barabarani kwenye wilaya zenu ili kuongeza mapato na kuboresha maisha ya wakulima na wachuuzi.

Kuna mengi mnayotakiwa kuyafanya na kuwa wabunifu wa kuongeza mapato na kubadilisha maisha ya wananchi wenu. Endeleeni kujifunza na kufahamu ziliko fursa na kuanza kuelekeza nguvu huko.

Kwa wakuu wa wilaya wanaoendelea na majukumu yao ni vyema kujihadhari na kawaida ya kuzoea madaraka na kujiona miungu watu. Kutumia ofisi zenu kukandamiza wananchi, kuropoka na kujisahau kuwa ninyi ni watumishi na uteuzi ukitenguliwa ni watu wa kawaida.

Wakuu wa wilaya tatueni matatizo ambayo watangulizi wenu hawakuyafanyia kazi. Malizeni viporo ambavyo ni mwiba kwa wananchi hasa vile vilivyokwama kwani waliokuwa na nafasi hizo kabla yenu hawakuvishughulikia.

Katika maeneo mengi mathalani wilaya zinazopakana au zilizo jirani na hifadhi kama Mkomazi, Serengeti na Mikumi misiba ya watu kupoteza maisha, mazao na mali kuharibiwa ni mingi. Vijijini wananchi wanalalamika kuuliwa au kujeruhiwa na tembo, fisi, nyati na mamba hivyo wakuu anzeni na hilo, kuwasiliana na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kurekebisha hali hiyo.

Mambo ni mengi lakini unyanyasaji wanawake na watoto, kuua na kujeruhi wazee kwa madai kuwa ni wachawi ni kero zinazoripotiwa ni vyema wakuu wa wilaya mkayashughulikia na umma ukaona haki ikitendeka na maisha yakibadilika. Viongozi tunawakumbusha mwisho wa uovu, kutesa wananchi, kudhulumu, kugombana na wenye itikadi tofauti na kupendelea ufisadi ni aibu, jihadharini na mambo yanayofanywa bila kumwogopa Mungu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






# Muungwana Lazima Nilonge

## Kuondoa kodi kwaweza kuwa mwarobaini ukosefu wa ajira

Na Askofu William Mwamalanga

**KUONDOA** kodi sumbufu kwa vijana wanaojiajiri, wanaomaliza shule na vyuo mbalimbali kwa miaka mitano ya mwanzo, kunaweza kuwa kivutio cha wengi wao wanaotaka kujitegemea kikazi.

Tatizo la ajira kwa vijana sasa hivi ni kubwa kuliko wakati mwingine na unahitajika ufumbuzi ambao mbinu mojawapo ni kuondoa kodi kwenye miradi yao. Kwa kufanya hivyo serikali itakuwa imeajiri wengi kwa haraka badala ya sasa vijana wengi kubaki kukodolea nafasi za ajira chache kwenye magazeti na hata uongozi wa kisiasa.

Mbinu hii inaweza kuwatengeneza walipa kodi wengi kwa muda mfupi ambao watakuwa wanachangia taifa lao baada ya miaka kadhaa ya uwekezaji.

Ni muhimu kutumia mbinu hii ambayo inaweza kuwatajirisha Watanzania kwa haraka na kuliinua taifa kiuchumi na kujipatia maendeleo kwani katika mpango huu vijana wengi watatumia mitaji midogo kutengeneza mikubwa.

Ndani ya muda mfupi taifa litakuwa na walipakodi walioandaliwa na kuingia kwenye dunia ya wafanyabiashara na kuchangia kodi kwa hiari kama ilivyo Japan, china, Canada, Ujerumani na mataifa mengine ya Magharibi.

Rais Samia Suluhu Hassan, pamoja na mwarobaini huu tunaoupendekeza ni vyema ukaona kuwa awamu hii ya nne iwe ya ustawi wa haki kwa Watanzania kuzifuta sheria kandamizi na mzigo kwa taifa hili.

Ikumbukwe kuwa baadhi yake zimetumiwa na watu wanaopata madaraka serikalini na kwenye siasa kupora mali ya nchi, kuhujumu maisha yao na kunyang'anya mali za watu kwa kutumia sheria ikiwamo ya uhujumu uchumi, utakatishaji wa mali na zile za ugaidi kutoka nchi za magharibi ambako hata hivyo hazitumiki.

Madhara makubwa ya sheria hizo katika kipindi cha awamu ya tano yamekuwa kuwanyima haki wananchi kumiliki utajiri wa fedha kwani hata akaunti zao zilichunguzwa na fedha kuchukuliwa, wapo waliobambikiwa kesi kinyume na sheria.

Mambo ya biashara za watu kuwa mashakani kimekuwa chanzo cha umaskini kwa baadhi ya Watanzania kwani sheria hizo hazikutakiwa kuendelea kuwapo kwani utajiri wa watu umechukuliwa na kuwanufaisha wachache.

Kitendo cha kumbambikizia kesi ya ugaidi, utakatishaji fedha au uhujumu uchumi kama ilivyotokea kwa watu wengi ambao wanaendelea kusota rumande si jambo jema.

Ni vyema serikali ikazitazama na kuziangalia sheria za Idara ya Uhamiaji kwenye eneo la wahamiaji haramu hasa wa Ethiopia ambalo limekuwa biashara kwa baadhi ya Watanzania ambao hufanya kazi ya kuwaficha kwa lengo la kuwasafirisha kwenda nchi za kusini mwa Afrika ili kupata fedha.

Sheria hiyo iendane na ile ya kimataifa ya kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu ili kudhibiti udhalilishaji na mienendo mingine inayosababisha binadamu kuuzwa kama bidhaa.

Ni muhimu kama taifa kusiwe na sheria itakayomaliza biashara ya watu hao ambao hufichwa kwenye mazingira hatarishi ambayo mara nyingi husababisha mateso na vifo ambavyo vinaweza kuzuiliwa.

Ikumbukwe kuwa hivi karibuni alikuja Rais wa Ethiopia na kuwaombea wahamiaji wake msamaha ili kurudishwa makwao. Kwa hiyo, ufike wakati kuwe na utaratibu wa kulipia kodi kwa wanaovuka mipaka hao kuwa na utaratibu unaokubalika na bara la Afrika kuliko ilivyo sasa.

Ni kwa sababu uvukaji wao ambao unaweza kuhatarisha maisha yao umegeuzwa kuwa utajiri kwa maofisa wa uhamiaji wachache na wafanyabiashara wasio na maadili.

Aidha, kuna malalamiko kuhusu usajili wa madhehebu nchini, pengine ni muhimu kiundwe chombo cha usajili wa taasisi za kidini pekee kama ilivyo kwa vyama vya siasa ili kuondokana na urasimu wa kusajili makanisa na misikiti.

Inaweza kuchukua miaka hadi 10 kukamilika usajili wake jambo linalotazamwa kama agenda ya serikali ya kuminya uhuru wa kuabudu ambao upo kikatiba.

TANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

# MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA KUTOA HUDUMA YA BIMA KWA AJILI YA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) KUMBUKUMBU NA: 0010006856

Kampuni ya mafuta na gesi ya TOTAL East Africa Midstream B.V., Tanzania, inaalika makampuni ya bima yenye uzoefu na sifa kutuma nia ya kuwa moja ya watoa huduma za Bima katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha shughuli za uhandisi, ujenzi, uendeshaji na usimamizi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi lililofukiwa ardhini na lililofunikwa ili kutunza joto linalokatisha nchi za Uganda na Tanzania na lenye mfumo wa umeme wa kulipasha joto, miundombinu ya juu ya ardhi na eneo la kuhifadhia mafuta lililo katika eneo la Chongoleani, karibu na bandari ya Tanga nchini Tanzania. Mradi wa EACOP ni Mradi unaowezeshwa kifedha na inategemewa wakopeshaji wanaweza kuhitaji kufahamu juu ya mpango wa bima na udhamini bima.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**
Mradi wa EACOP unahitaji mpango wa bima na udhamini bima wenye kujitosheleza katika kipindi chote cha Mradi Pamoja na sera za bima zinazojumuisha majanga yote yanayoweza kutokea kwa upande wa Tanzania ambayo itatolewa na mtoa huduma za Bima wa Kitanzania au Shirikisho la Watoa Huduma za Bima wa Kitanzania (ambapo watoa huduma za Bima wa Uganda watatoa sera zinazojumuisha majanga yote yanayoweza kutokea nchini Uganda). Mawanda ya kazi yanayotarajiwa ni:

- Utoaji wa sera kwa muda unaotakiwa, kushughulikia masuala yote yahusuyo usimamizi na kodi,
- Nia na kuonyesha uwezo wa kufanya kazi na makampuni makubwa ya madalali wa bima na dhamana ya bima kwa miradi mikubwa na yenye mchangamano,
- Makubaliano ya kufanya kazi na watoa huduma wa Uganda ili kurahisisha usimamizi katika nchi zote mbili pale inapohitajika,
- Kufuata katika nyanja zote matakwa ya wakopeshaji wa Mradi,
- Viwango bora vya huduma za sera za bima ikijumuisha mchakato wa madai wakati wote wa Mradi, kwa kuhakikisha usawa kamili na mpango madhubuti wa dhamana ya bima,na
- Kuhakikisha usawa kamili wa kisera zinazotolewa kwa ajili ya kuwekea bima mali za Mradi zilizo Tanzania kwa kushirikiana kwa ukaribu sana na watoa huduma wa bima au udalali wa bima wa Uganda.

**VIGEZO MUHIMU:**
Makampuni au shirikisho la makampuni linalo onyesha nia linaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili wa kampuni au shirika kwa ajili ya kutoa huduma tajwa katika nchi husika.
- Uzoefu wa kutoa huduma za bima katika miradi mikubwa ya viwanda na kwenye miradi yoyote ya mafuta na gesi.
- Uzoefu wa kufanya kazi katika mazingira ya kimataifa na kuwa na mtoa huduma wa dhamana ya bima wa kimataifa.
- Kuthibitisha uwezo wa kushirikiana na watoa huduma wabima wa Uganda ili kurahisisha utendaji.
- Uwezo wa kufanya kazi kwa ukaribu na dalali wa dhamana ya bima anayehusika na maswala ya udhamini wa bima.
- Uzoefu wa kusimamia sera na kufanyia kazi swala lolote la miongozo, ikiwemo kodi, kimsingi lakini sio tu kwenye utoaji wa sera ndani ya muda, kujibu maswali yote ya wanufaika katika kipindi chote cha Mradi, kusimamia madai na usimamizi wa sera.
- Uthibitisho wa uwepo wa rasilimali zinazofaa – watendaji wenye sifa na uzoefu (wenye ujuzi wa majanga makubwa na ya kipekee yanayoweza kutokea pamoja na udhamini wa bima) na timu Madhubuti kwa EACOP kwa maswala yote yanayohusiana na mpango kama huu wa bima na udhamini wa bima. Bainisha kiongozi wa timu (tafadhali wasilisha mchoro wa timu na uongozi Pamoja na wasifu wao, na).
- Uwezo wa kifedha wa kutekeleza huduma zinazohitajika.

---

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **EACOP.EOI-BROKERS@total.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00 jioni** Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **08 Julai 2021**

---

**Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).**

216320301

# Rais Samia awaapisha RC, RAS, wapewa maelekezo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan jana alimwapisha Balozi Batilda Salha Burian, kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora.

Aidha, Rais Samia alimwapisha Zuwena Omary Jiri kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, katika hafla fupi iliyofanyika Ikulu Chamwino mkoani Dodoma.

Akizungumza baada ya viongozi hao kuapishwa, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliwataka viongozi hao kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii ili kuwaletea maendeleo wananchi.

Majaliwa alitaka wasimamie huduma zinazotolewa na watumishi wao ili huduma hizo ziwe na ubora unaotegemewa na wananchi.

Aliwataka kuhakikisha watendaji katika maeneo wanayokwenda kusimamia rasilimali fedha zinazokwenda katika mikoa yao ili zitumike kama zilivyokusudiwa.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, alimtaka Balozi Batilda kusimamia mapato katika mkoa wake, kwa sababu kuna baadhi ya wilaya hazifanyi vizuri katika ukusanyaji wa mapato.

Kwa Mkoa wa Shinyanga, Ummy alimtaka Katibu Tawala wa Mkoa huo kusimamia vizuri matumizi ya fedha.




Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo (kulia), akikata utepe baada ya kukamilika kwa ujenzi wa ukuta wa Shule ya Msingi Makuburi ulijengwa kwa fedha za mfuko wa jimbo, alipofanya ziara mwishoni mwa wiki, kushoto ni Diwani wa Kata ya Makuburi, Shirima Olivery. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yataka sekta binafsi imara

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Kattanga, ameitaka sekta binafsi kufanya shughuli zake kwa kuzingatia misingi ya nidhamu, uwajibikaji na uwazi ili kuleta ufanisi zaidi kwa sekta hiyo ambayo ni injini muhimu kwa maendeleo na ukuaji wa uchumi.

Akizungumza kwenye mkutano wa kamati tendaji wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) ulifanyika mwishoni jijini Dar es Salaam ikiwa sehemu ya maandalizi ya mkutano wa 12 wa baraza hilo utakaoongozwa na mwenyekiti wa baraza na Rais Samia Suluhu Hassan wiki hii, Balozi Kattanga alisema dhamira ya serikali ya awamu ya sita ni kuwa na ukaribu zaidi na sekta binafsi.

"Serikali ya awamu ya sita imekuja na mbinu tofauti ambayo ni shirikishi katika kutekeleza miradi yake, tutashughulika na mtu au taasisi yoyote ambayo inafuata misingi ya nidhamu na uwajibikaji," alisema Balozi Kattanga ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya TNBC.

Aliitaka sekta binafsi na umma kubadilika kimtazamo na wote kufanya kazi kama timu na pale ambapo changamoto zitakapobainika, vikao vya kamati tendaji ambavyo wajumbe wake hutoka sekta binafsi na umma kukaa na kuja na majawabu ya pamoja.

"Serikali itaendelea kuweka mikakati yake vizuri ya kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara na uwekezaji sambamba na kutengeneza ajira kwa vijana, huduma za afya pamoja na elimu," alisema.

Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Dk. Godwill Wanga, amesema mkutano huo umepokea na kujadili mawasilisho matatu ya tafiti ambayo yalihusu kuendeleza viwanda vya misitu, kuboresha usimamizi wa kodi na namna ya kupanua wigo wa walipa kodi pamoja na nafasi za taasisi za udhibiti kusimamia badala ya kuwa washindani.

"Tumepokea mawasilisho matatu ambayo tumeyajadili na kuyapitisha kwa ajili ya kikao cha 12 cha baraza kitakachofanyika tarehe 26 Juni, 2021 chini ya Rais ambaye ndiye mwenyekiti wa baraza hilo," alisema.

Aliongezea kuwa wajumbe wa mkutano huo wameonyesha matumaini makubwa kwa hatua zinazochukuliwa na serikali katika kuifanya sekta binafsi inatoa mchango unaostahili kwenye ukuaji wa uchumi na pato la Taifa.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alisema mipango imewekwa kuhakikisha nchi inafikia uchumi wa juu kwa kuweka mazingira rafiki ikiwamo kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kwa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP).

"Tunahitaji kuwa na sekta binafsi yenye nguvu na ndiyo maana serikali inatekeleza miradi mingi kwa ubia na sekta hiyo na ili kuweka mazingira mazuri zaidi kwenye bajeti ya mwaka 2021/22 tumefuta baadhi ya kodi pamoja na kupunguza tozo mbalimbali," alisema Tutuba.

# FAO yasaidia vifaa vya kilimo milioni 124/-

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), limetoa msaada wa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 124, kwa wizara ya kilimo.

Vifaa hivyo vitawasaidia maofisa ugani kutekeleza majukumu yao na kuwatatulia wakulima kero.

Ofisa afya ya mimea kutoka FAO, Mushobozi Baitani, alisema msaada huo utakuwa suluhisho kwa maofisa ugani kuwafikia wakulima na kuwatatulia kero zinazowakabili.

Alisema msaada huo ni pikipiki, vishikwambi na vifaa mbalimbali vya kujikinga wanatekeleza majukumu yao ya kila siku.

Alisema, pikipiki zitawasaidia maofisa ugani kuwatembelea wakulima wao na kuwasaidia kulima kwa tija.

"Lakini kwa kutumia vishikwambi wataweza kupakua taarifa mbalimbali za mimea pamoja na magonjwa yanayoipata ili kupata suluhu kwa haraka," alisema.

Kadhalika, alisema kuwa vishikwambi hivyo watavitumia pia kutoa taarifa kwenye App ya kilimo mtandao ambayo itakuwa imeunganisha maofisa ugani pamoja na wataalamu mbalimbali.

"Ofisa ugani anapokwenda kutembelea wakulima na kukutana na kitu ambacho hakielewi anaweza kupiga picha na kutumia kwenye App ya kilimo mtandao ili kupata msaada, lakini anaweza kutafuta suluhu kwa kutumia kishikwambi hicho kwa magonjwa ya mimea," alisema.

Waziri wa Kilimo, Pro. Adolf Mkenda, akipokea msaada huo, aliishukuru FAO, kwa msaada huo, ambao umelenga vipaumbele vya serikali.

Alisema vipaumbele vya serikali katika sekta ya kilimo hivi sasa ni kuboresha utendaji wa maofisa ugani.

Alisema katika mwaka wa fedha wamepanga kununua na kugawa pikipiki 1,500 kwa maofisa ugani watakazozitumia kutekeleza majukumu yao.

Aidha, alisema kuwa pikipiki hizo zitawasaidia maofisa ugani kuwafikia wakulima katika maeneo mbalimbali na kuwasaidia katika kuboresha kilimo chao kuwa na tija.

Mwakilishi wa FAO, nchini Stephen Kargbo, alisema msaada huo ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za serikali ya Tanzania katika kuboresha shughuli za maofisa ugani.

# RC ataka usimamizi stakabadhi ghalani

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge, amewaagiza viongozi na wadau wa vyama vya ushirika kusimamia mapato ya halmashauri kupitia mazao yanayouzwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani.

Amesema lengo ni kuongeza tija na maduhuli ya serikali.

Ibuge alitoa agizo hilo wakati anazungumza katika kikao maalum cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Songea cha kujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Amesema mapato ya serikali na wakulima yamekuwa yanapotea kwa sababu ya usimamizi na ufuatiliaji mdogo kwa baadhi ya viongozi kutosimamia ipasavyo mazao yanayopaswa kuuzwa kwa mfumo wa stakabadhi ghalani, kitendo kinachosababisha halmashauri kukusanya chini ya kiwango kilichokusudiwa.

Aliagiza madiwani na watendaji kusimamia kwa umakini mkubwa uuzaji na ununuzi wa mazao ya wakulima kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani, ili waweze kuuza mazao hayo kwa bei yenye tija na wakulima kunufaika na kilimo wanacholima badala ya kulanguliwa mazao yao.

"Mfumo wa stakabadhi ghalani ni matakwa ya Ilani ya CCM, kipengele cha 34(i) kinazungumzia wakulima kuuza mazao ya stakabadhi ghalani. Pia umetolewa mwongozo wa mazao yanayotakiwa kuuzwa kwenye mfumo huu," alisisitiza Ibuge.

Amesikitishwa na kitendo cha baadhi ya walanguzi wa mazao maeneo ya vijijini kununua ufuta kilo moja kwa shilingi 500 kwa kilo, wakati kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani kilo moja inauzwa shilingi 1,400.

Mfumo wa stakabadhi ghalani unawataka wakulima wa ufuta, soya na mbaazi kuuza mazao yao kwenye vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS).

# Jumuiya kukabili mauaji ya wazee, wenye ualbino

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

JUMUIYA ya Ahmadiyya Muslimu Jamat Tanzania, imejitosa kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto wadogo na wanawake, mauaji ya vikongwe na watu wenye ualbino mkoa wa Shinyanga.

Katika hatua ya kwanza inajenga nyumba za ibada (misikiti) zaidi ya 20 kata zote zinazozunguka mkoa huo.

Hayo yalibainishwa jana na Amir na Mbashiri Mkuu wa jumuiya hiyo, Shekhe Tahir Mahmood Chaudhry, wakati wa mkutano mkuu wa jumuiya, uliofanyika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

Alisema moja ya sababu iliyosababisha kujenga nyumba za ibada mkoa wa Shinyanga ni uwapo wa imani za kishirikina zinazosababisha kuibuka kwa mauaji ya vikongwe na watu wenye ualbino, hivyo wameanza kwa kujenga nyumba hizo ili kuwajenga wananchi kiimani juu ya vitendo hivyo.

"Jumuiya hii, viongozi wake hawaruhusiwi kujiunga na chama chochote cha kisiasa, moja ya majukumu yetu ni kueneza dini kwenye maeneo yasiyokuwa na dini bila kuvunja sheria za nchi, kupambana na mauaji ya wazee, watu wenye ualbino na ukatili wa kijinsia," alisema Mahmood.

Katibu wa jumuiya hiyo, Shekhe Abdulrahman Ame, alisema licha ya kujenga nyumba za ibada, bado wamekuwa wakipeleka huduma ya majisafi na salama sehemu ambazo zina changamoto ya huduma hiyo kwa kushirikiana na serikali kwa kujenga visima virefu na vifupi.

Aidha, alisema wameshajenga na kukarabati zaidi ya visima 150 katika vijiji na kata vilivyopo mkoani Shinyanga, nakwamba huduma hiyo pia imetolewa katika mikoa ya Geita na Simiyu na wananchi wanapata huduma bila kujali itikadi za kidini.

Naye kiongozi wa jumuiya kwa upande wa wanawake, Zanana Omari, alisema wamekuwa wakianzisha kambi za malezi kipindi cha likizo kwa watoto wa miaka saba hadi 15 na kuwafundisha maadili na dini, na kwamba wanapokosa malezi wakiwa wadogo ukubwani ndio wakataji mapanga kwa wazee.

Zuhura Iddi, mkazi wa Salawe, alisema kabla ya uwapo wa visima hivyo, walikuwa wakitumia maji ya madibwi ambayo sio safi na salama, lakini kwa sasa vimepunguza changamoto ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma hiyo.

Shafii Ghari, kutoka Kenya, alisema kuwa alikuwa anashindwa kufika Tanzania akijua kuna mauaji ya vikongwe na watu wenye ualbino kwa kuhusishwa na inami za kishirikana, lakini baada ya jumuiya hiyo kujenga misikiti na kutoa elimu, amejisikia huru kuingia nchini.



Mkuu wa Wilaya ya Iringa Mjini, Mohamed Moyo, akila kiapo kwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga (kushoto), katika ukumbi wa Halmashauri ya Iringa Mjini jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wajibu wa wazazi kwa watoto waelezwa

**Na Cristina Mwakangale**

SERIKALI imesema wazazi wana jukumu la kuwalea watoto wao na kuwapatia maslahi na haki za msingi kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya maisha yao.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kigamboni, mkoani Dar es Salaam, Dalmia Mikaya, aliyasema hayo mwishoni kwa wiki kwenye kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika, inayoadhimishwa Juni 16, kila mwaka.

Alisema kuwa watoto wanapitia changamoto nyingi ikiwamo kunyanyaswa, mimba za utotoni pamoja na kutumia dawa za kulevya, vitendo ambavyo vinaharibu utu na hadhi yao kwenye jamii.

Mikaya alisema jamii inayowazunguka ikiongozwa na wazazi, walezi wanalo jukumu la kuungana pamoja kupinga vitendo vya unyanyasaji dhidi ya watoto na kushirikiana kuwalea kimaadili na elimu bora.

"Niwaombe wazazi na jamii kwa ujumla wakati tunaadhimisha siku hii ni wakati wetu sasa kuendelea kuwalinda watoto wetu kwa dhati dhidi ya ukatili wataofanyiwa na kuhakikisha wanatambua haki zao na kuzipata."

Diwani wa Mji Mwema, Omari Ngulangwa, alisema jamii ndiyo inayotakiwa kuwa na mabalozi wa kulinda haki za watoto, ili wawe katika maisha bora na salama zaidi akisema serikali ishirikiane na wadau kuona umuhimu wa kuilinda jamii.

Alisema baadhi ya watoto wanafanyishwa kazi mbalimbali za ndani, huku akiiasa jamii kuwa mabalozi wazuri na kulinda haki za watoto.

Meneja wa Baraza la Taifa la Watu wanaoishi na Virusi vya Ukimwi (NACOPHA) Kanda ya Dar es Salaam, Victoria Huburys, alisema wanathamini na kutambua umuhimu wa watoto katika maendeleo ya jamii.

Alisema mtoto ana haki ya kuishi na kupata afya njema, akisema serikali na wadau wote kuelekeza nguvu kubwa katika mabadiliko ya kisera, kisheria na kimfumo ili kujenga jamii yenye kujali na kutunza haki ya watoto.

Victoria alisema matokeo ya vitendo hivyo ni watoto kupata athari kisaikolojia, kuacha masomo, vifo, mimba za utotoni na hata kusababisha maambukizi ya magonjwa mbalimbali kama vile kuambukizwa Virusi Vya Ukimwi (VVU).

HABARI BUNGENI

# Mikakati mitatu kuharakisha mafao wastaafu

OFISI ya Waziri Mkuu imeainisha mikakati mitatu katika kuhakikisha watumishi waliostaafu wanapata mafao yao kwa wakati, ikiwamo kuwatambua wanachama.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, alitoa kauli hiyo bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kibaha Vijijini (CCM), Michael Mwakamo.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia watumishi waliostaafu kupata mafao yao kwa wakati.

Akijibu, Naibu Waziri Katambi alisema mikakati hiyo ni kutengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA ili kuwatambua wanachama wake na kulipa mafao stahiki pale wanapodai mafao.

"Kulipa malimbikizo mbalimbali ya mafao ya wanachama yaliyopaswa kulipwa na mifuko iliyounganishwa na yale yaliyopokelewa kipindi ambacho mchakato wa kuunganisha mifuko ulikuwa unaendelea," alisema.

Alitaja mkakati mwingine ni kuandaa ofisi mbalimbali nchini kote na kuweka misingi bora itakayowezesha utoaji wa huduma bora kwa wanachama wake ikiwa ni pamoja na kuimarisha mifumo ya malipo.

Alisema ili kuhakikisha wastaafu wanalipwa kwa wakati, waajiri wanakumbushwa kufuata kikamilifu utaratibu ulioainishwa katika Sheria namba 2 ya Mwaka 2018, ambapo inaelekeza ipasavyo maandalizi ya taarifa za wastaafu kabla ya malipo.

"Mifuko imeendelea kuboresha mifumo yake ambapo matarajio ni kuwa waajiri nao wafuate vizuri utaratibu ulioainishwa kisheria ili kupunguza ucheleweshaji wa kulipa mafao kwa wastaafu," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) ulianzishwa rasmi tarehe 1/8/2018 kwa Sheria Namba 2 ya Mwaka 2018.

Alisema mfuko huu ni matokeo ya kuunganisha mifuko minne (4) ya awali (LAPF, GEPF, PPF na PSPF) ambayo ilikuwa ikihudumia watumishi mbalimbali wa umma na kuufanya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kubaki ukihudumia sekta binafsi.



Mbunge wa Jimbo la Kibaha Vijijini, Michael Mwakamo, akiuliza swali Bungeni jijini Dodoma jana, kuwa serikali ina mpango gani kuwasaidia watumishi waliostaafu kupata mafao yao kwa wakati. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bil. 3/- zakusanywa uvuvi wa bahari kuu

SERIKALI imesema Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu imekusanya zaidi ya Sh. bilioni 3.091 ndani ya kipindi cha miaka mitano. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alieleza hayo bungeni jana wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum(CCM), Angelina Malembeka.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji ni asilimia ngapi ya mapato yatokanayo na uvuvi wa Bahari Kuu inaenda upande wa Zanzibar na kutaka kujua kwa miaka tano iliyopita, Zanzibar imepata kiasi gani. Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Ulega alisema fedha hizo zimekusanywa kuanzia mwaka 2017 hadi Machi 2021 huku Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikipata mgawo wa zaidi ya Sh. milioni 618.

Hata hivyo, alisema mgawanyo wa mapato yatokanayo na uvuvi wa Bahari Kuu unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu namba tano ya mwaka 2020 Kifungu namba 79 ambayo inaelekeza mgawanyo wa mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu kwa utaratibu maalum.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar asilimia 20, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania asilimia 30 na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi Bahari Kuu asilimia 50.

# Uzalishaji wa mbegu sasa watengewa bajeti

BUNGE limeelezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/22, serikali imetenga Sh.milioni 60 kwa ajili ya kuzalisha mbegu za aina 56 za miti ya asili ikiwamo mninga.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, aliitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Sikonge (CCM), Joseph Kakunda.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali itazalisha mbegu za mninga ili wananchi waweze kupanda na kuzalisha miti hiyo kibiashara.

Akijibu, Naibu Waziri huyo alikiri serikali inatambua umaarufu wa mti wa mninga katika matumizi ya shughuli za ujenzi na utengenezaji wa samani.

Alisema kutokana na umuhimu huo, wizara kupitia Wakala wa Misitu (TFS) imeandaa mpango wa miaka mitano wa kuendeleza mti huo na miti mingine kibiashara kwa kuipanda kama ilivyo miti ya kigeni.

Alibainisha mpango huo unahusisha aina 56 za miti ya asili ikiwamo mninga ambapo tayari fedha zimetengwa kwa kazi hiyo.

Alisema nia ya wizara ni kuongeza kasi ya uzalishaji wa mbegu za miti ya asili ili wananchi waweze kuzipata kwa urahisi kupitia TFS zilizopo kwenye kanda mbalimbali hapa nchini.

"Wizara itaendelea kuimarisha elimu ya upandaji wa mti wa mninga ili kuleta hamasa ya kupanda na kutunza miti hiyo na serikali itahakikisha elimu ya utunzaji na uendelezaji wa miti ya mninga iliyopo katika maeneo ya mashamba ya wananchi inatolewa ili miti hiyo itunzwe kwa ajili ya kuzalisha mbegu ili kuwezesha wananchi kupanda miti ya mninga kibiashara," alisema.



Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 22, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI


Ukurasa 14

## Waathirika wanapohoji kulikoni wabakaji wanapewe dhamana


Ukurasa 12

Ndizo salamu za wadau shule mchanganyiko


Ukurasa 13

KIPANGA DAUDI NI 'ATLASI' INAYOISHI

TEKNOLOJIA
**NA SABATO KASIKA**

# Walimu, familia wanavyowapika watoto kuibua vipaji, ubunifu

• Mtoto aunda roboti ya maboksi



Mwanafunzi Markus Mbaga akionyesha roboti ya maboksi aliyoiunda. **PICHA: SABATO KASIKA**

MARKUS Mbaga ni mwafunzi wa darasa la tatu katika Shule ya Msingi Genesis ya jijini Dar es Salaam, ambaye licha ya umri wake mdogo wa miaka tisa, ni miongoni mwa wanafunzi wanaong'ara katika maonyesho ya 'Siku ya Mradi wa Sayansi'.

Maonyesho hayo yaliyomalizika hivi karibuni shuleni Genesis, yalivutia wengi walioshuhudia wanafunzi wakionyesha vipaji vyao, vikiwamo vya ubunifu na pia kuchambua mada mbalimbali.

Kila aliyeshiriki 'Siku ya Mradi wa Sayansi' alijitahidi kuonyesha kile alichofundishwa lakini Markus anaibuka na roboti ya maboksi inayonyanyua na kuhamisha vitu mbalimbali kutoka sehemu moja kwenda nyingine, licha ya kuonekana kuwa ni nyepesi iliyoundwa kwa makaratasi.

Roboti hiyo ilivuta wengi waliokuwapo na kutamani kuona jinsi inavyofanya kazi. Kivutio zaidi ni mwanafunzi huyo anavyofahamu kujieleza akisema, anatamani kuwa mhandisi mkubwa hapo baadaye kama alivyo baba yake.

"Baba yangu ni mhandisi wa mitambo, amenifundisha kutengeneza roboti ya maboksi inayoshika kitu na kukihamishia kutoka sehemu moja hadi nyingine. Ndoto yangu ni kuja kusoma sayansi ili niwe mhandisi kama baba," anasema Markus.

Mwanafunzi huyo anasema amefanikiwa kutengeneza roboti hiyo, kwa vile amekuwa akitamani kuwa kama baba yake, na kwamba aliitengeneza namna alivyoelekezwa na alijifunza hadi kuikamilisha.

Mbali na mgunduzi wa roboti ya maboksi wanafunzi wengine walionyesha ubunifu wao ukiwamo wa kutengeneza satelait na vifaa vinavyotumia nguvu ya jua (sola), wapo waliotengeneza viburudisho kama chokoleti, juisi na bidhaa mbalimbali.

**MWANZO WA MAONYESHO**

Meneja wa Shule za Genesis, Joachim Jovin, anasema, katika kuibua vipaji vya wanafunzi shule iliamua kushirikisha wazazi na walezi kuwaelekeza kuvitambua na kusaidia kuviendeleza.

"Tulifanya hivyo, kwani wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao hutaka watoto wafuate kile walichojifunza na kazi wanazofanya, jambo ambalo wakati mwingine linaweza kuwa gumu, ndiyo maana tukaona kuna haja ya kuwashirikisha," anasema Jovin.

Anasema, si vibaya watoto kufuata taaluma za wazazi wao kama huyo Markus Mbaga ambaye baba yake ni mhandisi wa mitambo na kwamba hilo lifanyike kwa kupenda na si kwa kulazimishwa.

Meneja huyo anasema, katika shule yao, wana utaratibu wa kupeleka topiki kwa kila darasa ili kila mwanafunzi achague anayoitaka, ambapo anaifanyia kazi na kwamba anachoonyesha kukimudu ndicho kinachoendelezwa.

"Sisi tumeamua kuunga mkono mkakati wa serikali wa kutaka kuimarisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika shule, ndiyo maana tunahimiza ubunifu na uthubutu katika dhana nzima ya kukuza vipaji kwa manufaa ya taifa," anasema.

Anaeleza kuwa wanaibua na kuendeleza vipaji vya wanafunzi wao kuanzia darasa la kwanza hadi la saba, na kuongeza kipaji kikiendelezwa kwa miaka saba, mwanafunzi anahitimu elimu ya msingi akiwa na ujuzi wa kutosha.

**MBINU ZINAZOTUMIWA**

Aidha, mzazi au mlezi anatakiwa kujenga ukaribu na mtoto wake, kutenga muda wa kumfuatilia na kumwangalia anapocheza lakini kumjibu maswali kadri anavyouliza.

"Hivyo moja ya majukumu ya wazazi na walezi ni kulea na kuendeleza vipaji vya watoto wao, kwa vile ndiyo watu wa mwanzo wa kuibua, kupalilia na kuvikuza ndani yao," anasema.

Halikadhalika anataja umuhimu wa mzazi na mlezi kuwa karibu na mtoto kunasaidia kujua ni wapi kipaji chake kilipojificha na kuanza kumsaidia kukikuza kulingana na kipaji chenyewe na kwamba ndivyo hata wao wamefanya kwa wanafunzi wao kwa kushirikisha wazazi na walezi wao.

**INAENDELEA UK.13**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Ndizo salamu za wadau shule mchanganyiko kwa serikali

SHULE ambazo zinatoa elimu jumuishi zinazofundisha wanafunzi wazima na wenye ulemavu, nyingi zinakabiliwa na upungufu wa walimu maalum kwa ajili ya kuhudumia kundi hilo lenye mahitaji maalum.

Shule ya Msingi Buhangija jumuishi iliyopo Ibinzamata Manispaa ya Shinyanga, ni miongoni mwa zenye wanafunzi mchanganyiko, wakiwamo wenye mahitaji maalumu, na ni moja ya shule zinazokabiliwa na changamoto ya upungufu wa walimu maalum, kwa ajili ya kufundisha wanafunzi wenye ulemavu. Hatua hiyo inaleta ugumu katika ufundishaji.

Mwalimu Mkuu Fatuma Jilala, anasema shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 1,049 na wanaoishi na ulemavu wapo 227 wakati walimu ni 19, lakini wenye taaluma maalum wapo 10 pekee na hivyo kufanya kuwapo na upungufu wa walimu wanane.

Anafafanua kuwa wanaofundisha wanafunzi wenye uoni hafifu ni wanne, uhitaji ukiwa mwalimu mmoja, wasiosikia wako walimu sita na wanaohitajika ni saba na kwamba kutokana na upungufu huu wa walimu maalum, inakuwa vigumu kuwahudumia wanafunzi wenye ulemavu na hata waliopo inabidi wafanye kazi ya ziada ya kuwafundisha.

"Tunaomba awamu ya sita itupatie walimu wenye taaluma maalum, ili tuendelee kufanya vizuri kitaaluma, sababu shule inapokuwa na upungufu wa walimu tunapata shida katika ufundishaji kulingana na hali pamoja na mahitaji yao maalumu," anaongeza Jilala.

Shule ya Msingi ya binafsi ya Brother's iliyoko Kitangili Manispaa ya Shinyanga, ni miongoni mwa shule zinazofundisha watoto wenye mahitaji maalumu. Mwalimu Mkuu wa Brother's Fransisco Bega anasema wanafundisha watoto zaidi ya 30 wenye mtindio wa ubongo.

Anaongeza kuwa kutokana na ukosefu na upatikanaji wa walimu waliosomea taaluma hiyo, wanafunzi hao wanahudumiwa na walimu wawili pekee.

"Hapa shuleni kwetu tuna uhitaji mkubwa wa walimu maalum, lakini hawapatikani. Kuna maelezo kuwa ni wachache sana waliosomea taaluma hii," anasema Bega na kuongeza: "Wanafunzi hawa wenye ulemavu



Wanafunzi wenye uoni hafifu wakijadiliana na Nipashe kuhusu masomo na matatizo yanayowakumba. **PICHA: MARCO MADUHU**

> Inafika kipindi unachoka kufundisha, lakini ukiangalia hawa watoto wanahitaji msaada wetu ili watimize ndoto zao, kwa hiyo inabidi ujikaze kufundisha na wafikie malengo yao.

ufundishaji wao unahitaji umaskini na upendo sana kulingana na hali zao, hivyo mkiwa walimu wachache inafika kipindi mnachoka kufundisha."

Mmoja wa walimu wa shule hiyo, Anna Geofrey, anasema wanafunzi hao wenye utindio wa ubongo, wana matatizo mengi, hasa wale ambao wana anza masomo ambao hawawezi kujihudumia na hujiendea haja kubwa na ndogo.

Anasema kutokana na uchache wa walimu, inawawia vigumu kufundisha kikamilifu, huku wakiwasaidia na kuwasafisha wale ambao watakuwa wamejisaidia.

"Tunapokuwa walimu wachache kufundisha wanafunzi hawa wenye ulemavu, inafika kipindi unachoka kabisa na hivyo kutokuwa na hamu ya kufundisha ni kwa sababu ili wapate kuelewa inahitajika mwalimu utulize akili yako kikamilifu na uwe huru," anasema Anna.

Agnes Makambajeki ni mwalimu maalum, ambaye anafundisha wanafunzi wenye tatizo kama lake la uoni hafifu katika Shule ya Msingi Buhangija, anasema tatizo hilo la upungufu wa walimu maalum shuleni hapo limekuwa likiwalazimisha kufanya kazi kupita kiasi.

Anasema kutokana na kuwapo walimu 10 pekee shuleni hapo wenye taaluma maalum, imewabidi wajipange vizuri kufundisha wanafunzi hao wenye ulemavu, ili wapate kuwasaidia kutimiza ndoto zao kama alivyotimiza ya kwake.

"Inafika kipindi unachoka kufundisha, lakini ukiangalia hawa watoto wanahitaji msaada wetu ili watimize ndoto zao, kwa hiyo inabidi ujikaze kufundisha na wafikie malengo yao," anasema Makambajeki.

Mwanafunzi mwenye uoni hafifu Modesta Daudi, ambaye anasoma darasa la nne katika Shule ya Msingi Buhangija, anasema tatizo la upungufu wa walimu limekuwa likiwapa changamoto kuelewa masomo.

Anasema inafikia kipindi wanafunzi wenye ulemavu wanachanganywa na wazima darasa moja, huku mwalimu ambaye anafundisha ni yule asiye na taaluma maalum hivyo kusababisha wenye mahitaji maalumu washindwe kuelewa.

"Unapotuchanganya sisi wanafunzi wenye ulemavu darasa moja na wazima na mwalimu anayefundisha hana taaluma maalum, hapo tutaelewa vipi masomo?" ana hoji Modesta.

"Tunachoomba kwa serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyesema ataajiri walimu tunaomba atupatie walimu wa kutosha wenye taaluma maalum, ili tupate kuelewa masomo na kufanya vizuri kitaaluma," anaomba Modesta.

Diwani wa Ibinzamata ilipo shule hiyo, Ezekiel Sabo, anasema amekuwa akipiga kelele kwenye Baraza la Madiwani kulalamikia upungufu wa walimu maalum shuleni hapo.

Anasema haiwezekani wanafunzi wenye ulemavu kuchanganywa na kufundishwa darasa moja na wazima, tena na mwalimu ambaye hana taaluma maalumu na wakati mwingine asiyejua lugha ya alama.

"Naiomba sana serikali kama tunahitaji kuwanyanyua kitaaluma wanafunzi hawa wenye ulemavu, basi ifundishe na kuajiri walimu wa kutosha wenye taaluma maalum na siyo kufanya mambo ambayo hayatawasaidia watoto hawa," anashauiri Sabo.

Ofisa Elimu Shule za Msingi Manispaa ya Shinyanga, Neema Mkanga, anasema tayari wameshaomba kupatiwa walimu wapya wakiwamo wenye taaluma maalum na kufafanua kuwa suala la wanafunzi wenye ulemavu kuchanganywa darasa moja na wazima ni sera ya taifa.

Anaongeza kuwa mwongozo umeshatolewa kutoka Wizara ya Elimu kuwa wanafunzi hao wenye mahitaji maalum wasitengwe na wenzao bali wachanganyike na iwe elimu jumuishi.

Anasema wakiwatenga na wenzao ni sawa na kuwabagua hivyo wanalazimika kuwa changamanisha kwenye darasa moja na kufundishwa pamoja, ambapo akitoka mwalimu kufundisha asiye na taaluma maalum, anaingia mwenye taaluma hiyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Ummy Mwalimu, Mei 9, mwaka huu, alitangaza ajira za walimu 6,949, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma na shule zenye mahitaji maalumu linangojea lakini kwa kuona kuwa walimu wenye taaluma maalumu wanapatikana kwenye shule zao.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Kipanga Daudi ni 'Atlas' inayoishi

- Mkali kuhifadhi mambo makubwa, majina ya marais
- Anaomba asaidiwe, kuinua wenye mahitaji maalum

DAUDI Mwigamba mwanafunzi wa kidato cha sita mwenye kipaji maalumu cha kuhifadhi mambo mengi akilini kuanzia majina ya mataifa yote duniani, viongozi wake wakuu na miji mikuu akifanya hivyo kuanzia akiwa na miaka 10, unaweza kumfananisha na Atlasi inayoishi.

Anaweza kufananishwa na Atlasi au kitabu cha ramani chenye uhai, kutokana na kuhifadhi mambo yote muhimu yaliyo kwenye vitabu hivyo kichwani kwake.

Anasema hata akiamshwa usingizini na kuulizwa jina la kiongozi yeyote duniani, au mji mkuu wa taifa lolote ama hata kutakiwa kutaja majina ya nchi katika bara fulani hasumbuki, kwani jibu analo kwenye ulimi.

Aidha, anasema anafanya hivyo si kwa kujifunza kwa nguvu wala kutumia juhudi kubwa kwa sababu ana kipaji cha kuhifadhi masuala hayo na ili kisipotee anaomba wadau wamsaidie kumwendeleza kwenye eneo hilo.

Anasema anatamani kutumia kipaji chake kujua mambo mengi na makubwa zaidi kiasi atakavyopewa fursa, lakini anatarajia kuongea na kuhamasisha kujifunza kwa bidii, kujiamini na kuwapa matumaini watu wengi hasa wenye mahitaji maalumu kuwa kila kitu kinawezekana na waache kujinyanyapaa wenyewe.

Anasema licha ya kuishi na albinism anajiamini na anafahamu kuwa ni mtu kama walivyo wengine na angeomba wadau wamsaidie ili afike kwenye majukwaa mbalimbali kuulizwa maswali na kuyajibu papo kwa papo kwa ufasaha ili kuwaonyesha wanaoishi na ulemavu wengine na Watanzania kuwa kila kitu kinawezekana nao wanaweza kukifanya tena kwa ufasaha zaidi.

Daudi anayesoma kidato cha sita kwenye Sekondari ya Tusiime Dar es Salaam, anaeleza kuwa anapoulizwa swali mathalani ni nani Rais wa Trinidad and Tobago anasema ni mwana mama Paula-Mae Weekes.

Anaongeza kuwa pengine wanafunzi wengi, walimu wa Jiografia na hata idadi kubwa ya Watanzania hawafahamu kuwa kuna mataifa madogo kama Tuvaluu, Tonga, Kiribati na Papua New Guinea, lakini yeye anayajua na amehifadhi taarifa zake zote akilini.

"Ninapenda kuonyesha wengine wakiwamo wenye mahitaji maalumu kuwa tunaweza kuongea kwa ufasaha, kusikia kikamilifu, kujiamini, kuongea na hadhara na kuonyesha kuwa mwenye mahitaji maalumu anaweza kufanya jambo tena vizuri na kwa ukamilifu zaidi," anaongeza mwanafunzi huyo anayesoma Fizikia, Kemia na Hisabati (PCM).

Anataja kuwa yuko miongoni mwa wanafunzi watano bora darasani kwake na anatarajia kujitahidi kwenye masomo yake ya kidato cha sita ili kusoma uhandisi.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, anasema anatamani kukutana na wanafunzi wenzake wa shule za umma na binafsi, sekondari na hata za msingi makundi mbalimbali kama wasomi wa vyuo vikuu na watoto walio katika mazingira magumu.

Anatamani kufika mbali hata bungeni, kwenye mikusanyiko mingine ya kitaaluma na kijamii na kuulizwa maswali yanayohusu majina ya mataifa, marais, au waziri mkuu, wafalme, miji mikuu na kingine chochote kuhusu nchi hizo na wahusika waone atakavyojibu kwa ufasaha papo kwa papo.



Daudi Mwigamba akiwa katika mahojiano na Nipashe hivi karibuni. N**A MPIGAPICHA WETU**

### ANACHOTAMANI KUFIKIA

Daudi anayesoma PCM anatamani kujikita kwenye uhandisi wa kompyuta (computer engineering) akilenga kusaidia kuandaa program mbalimbali zikiwamo za kusaidia watu wenye mahitaji maalumu mfano wenye uoni hafifu walioko vijijini na mazingira magumu na wale ambao kutokana na ulemavu walio nao wanashindwa kutumia vifaa vya kielektroniki.

"Ni kusaidia kama ikiwezekana kupunguza pengo la kidijitali lililoko baina ya watu wenye mahitaji maalumu na jamii nyingine yenye viungo vilivyokamilika," anasema mwanafunzi huyo.

### ANAPOTOKEA

Daudi anasema kipaji chake kilianza kujitokeza kwa mara ya kwanza akiwa darasa la nne baada ya mama yake kumnunulia Atlasi na kwa wiki mbili aliweza kuhifadhi majina ya mataifa yote 52 ya Afrika, miji mikuu na wanaoyaongoza.

> Ninapenda kuonyesha wengine wakiwamo wenye mahitaji maalumu kuwa tunaweza kuongea kwa ufasaha.

"Kipaji changu kilizidi kuimarika nilipokuwa kidato cha kwanza nilihifadhi majina ya mataifa yote duniani, viongozi wake, marais, wafalme na mawaziri wakuu. Nilikuwa nikiitwa mbele wakati wa mahafali ili wageni, wazazi na walezi waniulize maswali ya majina yawe ya nchi, viongozi na majiji makuu. Niliyajibu kwa ufasaha, wapo walionizawadia na kunipongeza," anasema Daudi.

### ALIYEMWIBUA/KUMWENDELEZA

Daudi anamtaja Meneja wa Shule za Tusiime Jane Katagira, kuwa ndiye aliyemwibua na kumtaka atumie kipaji hicho kutangaza uwezo wake wa kuelewa kwa kumshirikisha kwenye shughuli mbalimbali, akimpa fursa ya kuulizwa maswali yanayohusu eneo hilo ili kunadi kipaji chake.

Ninatamani kujua zaidi na kuwa pengine mtu wa kwanza duniani anayefahamu majina ya mataifa yote, viongozi wake, miji mikuu na pia 'physical features' akimaanisha vitu kama milima, mito, mabonde, maziwa, ghuba, misitu na majangwa.

Analenga kuwa 'atlasi' inayoishi na ramani ya dunia inayotembea na kuzungumza na watu mbalimbali kuhamasisha kila mwenye kipaji kukiendeleza na kwa wanaoishi na changamoto kujiamini na kujua kuwa kama mwingine anaweza kufanya jambo mwingine hata wewe unaweza kulifanya kwa umahiri zaidi.

***Anawaomba wanaotaka kumsaidia kuwasiliana na uongozi wa shule ya Tusiime, Nipashe au kumpigia simu yake namba 0736-056781.***

## Walimu, familia wanavyowapika watoto kuibua vipaji, ubunifu

**INATOKA UK.11**

Halikadhalika anataja umuhimu wa mzazi na mlezi kuwa karibu na mtoto kunasaidia kujua ni wapi kipaji chake kilipojificha na kuanza kumsaidia kukikuza kulingana na kipaji chenyewe na kwamba ndivyo hata wao wamefanya kwa wanafunzi wao kwa kushirikisha wazazi na walezi wao.

Lakini, anatoa angalizo kuwa, mzazi asimdanganye mtoto au kumpa jibu ambalo hana uhakika nalo na kwamba kama hana majibu amwambie ili naye katika maisha yake awe mkweli.

Meneja huyo anaongeza kuwa, katika dunia ya leo yenye ushindani, yanahitajika maandalizi ya kukuza vipaji vya watoto, ili wawe katika nafasi nzuri ya kushindana na wengine.

Jovin anasema, shule zao zimeamua kurejesha wazo la Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere la elimu ya kujitegemea kwa kuibua vipaji, kuviendeleza ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda vidogo shuleni vikiwamo vya kujifunza kukamua matunda.

Anasema, kuanzia Agosti mwaka huu, wataanzisha kilimo, ufugaji, ushonaji na pia viwanda vidogo shuleni ili kusaidia wanafunzi hata wanapohitimu elimu ya msingi waweze kujitegemea.

Katika maonyesho hayo mwanafunzi Giovanna Johnson, mwenye miaka tisa alitengeneza chokoleti na Jovin, anamwelezea kuwa anaweza kuhitimu elimu ya msingi akawekeza eneo hilo.

"Vilevile tuna mpango wa kutembelea wanafunzi wa shule za serikali ili wanafunzi wetu waweze kuonyesha vipaji vyao, lakini pia kujifunza kwa wenzao wa shule hizo iwapo watapewa idhini," anasema

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

# Waathirika wanapohoji kulikoni wabakaji wanapewe dhamana

LICHA ya Zanzibar kuwa na Sheria ya Ushahidi Namba 9 ya mwaka 2016, inayowanyima dhamana washtakiwa wa kesi za udhalilishaji wa kijinsia hasa ubakaji na ulawiti, kinachoendelea ni baadhi ya washtakiwa wa kesi hizo hupewa dhamana.

Hali hiyo, sasa inatajwa kuwa kichocheo cha kuongezeka kwa vitendo hivyo huku watoto na wanawake wakiwa waathirika wakubwa na hao wanahoji kulikoni.

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, inasema matukio 1,363 ya udhalilishaji wa kijinsia yaliyokusanywa na Jeshi la Polisi mwaka 2020 yanaonyesha ukubwa wa tatizo hilo.

### KWANINI WANADHAMINIWA

Kitendo cha kupewa dhamana kwa baadhi ya washtakiwa kimeibua mjadala kwa wanaharakati wa kutetea haki za wanawake, watoto na waathirika wa madhila hayo.

Baadhi ya wazazi wa watoto waliodhalilishwa wanalalamikia kuwepo kwa dhamana kwa watuhumiwa wa vitendo hivyo hali inayotoa mwanya kwa wahusika kuendeleza uovu.

Waathirika wa matukio hayo wanasema kinachoumiza zaidi ni kuwaona washtakiwa au watuhumiwa wa kesi hizo wakiwa nje kwa dhamana wakati sheria inawanyima dhamana.

### VILIO WALIODHALILISHWA

Ali Khamis (sio jina lake) ni miongoni mwa wazazi ambao watoto wao, walilawitiwa na kubakwa. Mwanawe wa kike mwenye miaka 15 (jina tunalihifadhi), ni mwathirika. Mzazi huyo anasema anashangaa kumwona mshtakiwa aliyemharibia maisha mtoto wake yupo mtaani anadunda wakati alishaikabidhi kesi hiyo katika vyombo vya sheria.

Aidha, anasema watuhumiwa hao wa kesi hizo wanapokuwa mitaani huleta vitisho kwa waathirika na familia zao na kuwafanya wazidi kuwa wanyonge na kudhani kuwa hawana wa kuwatetea kwa vile sheria inavunjwa wakati ndilo tegemeo lao.

"Mtuhumiwa aliyeniharibia mtoto wangu kwa kumbaka na kumlawiti leo hii yupo mtaani licha ya kumkabidhi katika vyombo vya sheria na nimekuwa na hofu kwani amekuwa akinipa vitisho mara kwa mara," anasema.

"Nashangaa sheria imeshaeleza kuwa kesi hizo hazina dhamana inakuwaje watuhumiwa hao wanapewa dhamana?" anahoji.

Fatma Abuu (japo sio jina halisi) ni mama wa mtoto aliyefanyiwa udhalilishaji, anayesema ni vyema sheria ikafuatwa na washtakiwa wasipatiwe dhamana kwani kitendo cha kupewa dhamana kinawaathiri kwa sababu ni watu wa karibu katika familia.

Mariyam Khamis Issa, mlezi wa mtoto aliyebakwa, ameziomba mahakama kuharakisha upatikanaji wa hukumu za kesi za udhalilishaji ili kuondoa mwanya wa kufanyika vitendo vya rushwa katika vyombo hivyo vya kusimamia haki.

Anasema bado kuna mlolongo mrefu wakati wa ufuatiliaji wa kesi hizo hali inayosababisha uwepo wa rushwa na kwamba amekuwa akifuatilia kesi zao kwa muda mrefu bila ya kutolewa hukumu na hatimaye watuhumiwa kuachiwa huru jambo linalosababisha kuwa na dhana ya kufanyika vitendo vya ufisadi mahakamani.

Makame Omar ambaye watoto wake wawili wamedhalilishwa na baba wa kambo, anasema baadhi ya watuhumiwa wanapopewa dhamana wanakuwa na kejeli na dharau mbele ya walioathirika na vitendo hivyo.

Anasema ili kupunguza machungu ya madhara yaliyompata ni vyema mahakama kutotoa dhamana kwa watuhumiwa wa vitendo vya udhalilishaji.

Meneja Mipango kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Ali Abdallah, anawataka watendaji wanaoshughulikia kesi za udhalilishaji kuacha muhali katika usimamizi wa sheria.

"Sheria ipo ya kuwa washtakiwa wa kesi hizi kutopewa dhamana sasa inakuwaje wanapewa dhama jambo hilo linarejesha nyuma juhudi za wananchi na wanaharakati wa kupinga vitendo vya udhalilishaji," alisema.

> "Ili kupunguza machungu ya madhara yaliyompata ni vyema mahakama kutotoa dhamana kwa watuhumiwa wa vitendo vya udhalilishaji.

### HAKIMU AJIBU

Hakimu wa Dhamana wa Mkoa wa Kusini Unguja, Kahmis Ali Simai, anasema kisheria mahakama haijafuta kifungu cha Jaji Mkuu kutoa dhamana katika Mahakama Kuu hivyo baadhi ya washtakiwa wanapatiwa dhamana kutokana na sababu maalum.

Anasema kuwa baadhi yao hulazimika kupewa dhamana kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za kiafya na kwamba washtakiwa wa kesi hizo huwa na matatizo ya kiafya ikiwamo ugonjwa wa kisukari na VVU.

Hakimu huyo anasema watu hao wanatumia dawa za kufifisha makali ya VVU na vyakula maalum hivyo kuendelea kuwaweka mahabusu ni kuwazidishia maradhi na hata kutishia maisha yao.

"Kwa mfano kuna mtuhumiwa alikuwa anajiandaa kufanya mtihani wa kidato cha sita, sasa usipompa dhamana unaweza kumkosesha haki zake nyingine za msingi kama elimu," anasema Simai.

Aidha, kwa mujibu wa maelezo yake si kila mshtakiwa wa kesi hizo huwa na hatia hivyo unapomkosesha kufanya mtihani wake wa shule endapo mahakama ikimwona hana hatia itakuwa ameumizwa kitaaluma.

Anasema kinachofanywa na Mahakama Kuu kipo kisheria na ni maelekezo ya utaratibu, hivyo ikiwa watu hawajaridhika na suala la dhamana wanapaswa kukata rufani.

Ofisa Mipango Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar, Thabit Abdalah Juma, anawataka wananchi kutambua kuwa kutoa hukumu katika kesi za udhalilishaji sio jambo rahisi kwani kupatikana na hatia kunachochukua muda mrefu ili kuepusha hatia zisizostahili.

Hivi karibuni Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema hajaridhishwa na utendaji wa Jeshi la Polisi katika kushughulikia kesi za udhalilishaji wa kijinsia.

Anasema yapo malalamiko kutoka kwa jamii kwamba Jeshi la Polisi limekuwa likifanya upatanishi wa suluhu wa kesi hizo katika vituo vyake na kuzimaliza kienyeji, yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi.

Akizungumza na wananchi pamoja na wanachama wa CCM Mkoa wa Mjini Magharibi hivi karibuni anasema wanachokifanya polisi sio kazi yao kwa mujibu wa sheria kwani wanatakiwa kuhakikisha wanatayarisha kesi kwa kufanya upelelezi na kuzipeleka mahakamani.

"Nilikutana na viongozi wa Jeshi la Polisi, Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na mahakama na kuwataka wakutane na kuweka utaratibu bora utakaohakikisha kesi hizo zinasikilizwa haraka ili jamii iondokane na malalamiko," anasema.

Rais Mwinyi aliwapongeza wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kufanya marekebisho bora katika sheria za udhalilishaji ambazo mtuhumiwa wa makosa hayo asipewe dhamana.



Dk. Mwinyi Talib Haji, Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, ofisi yake isikie kilio hicho na kupata ufumbuzi ambao hautawaathiri walalamikaji. **PICHA: MTANDAO**



## HABARI DODOMA

## Wataka udhibiti uvamizi wa ranchi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuchukua hatua za haraka kudhibiti wananchi wanaovamia kwenye vitalu vya ranchi za taifa, kwa kuwa ni miongoni mwa vikwazo katika uendelezaji wa sekta ya mifugo.

Wawekezaji wazawa katika vitalu hivyo walitoa ombi hilo kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alipokutana nao kwenye kikao kilichoandaliwa na Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), jijini hapa.

Mwenyekiti wa wawekezaji hao, Jackson Mwasonga, alisema kuwa wavamizi wanakwamisha shughuli zao na kuna wakati wanalazimika kutoa fedha kwa wavamizi ili kuchunga mifugo yao katika maeneo wanayomiliki kihalali.

Alisema suala hilo linawapa wakati mgumu sana ndio na kuomba serikali ichukue hatua.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Ranchi ya vitalu vya Kagoma yenye vitalu 16, Faustine Lutahoile, alisema: "Uvamizi unatishia maisha yao na mali zao wanaomba watoe tamko la kuwaondoa wavamizi ili waweze kufanya ufugaji unaohitajika kwa amani."

Mwekezaji wa Ranchi ya Kitengule mkoani Kagera, Projestus Gamasho, alisema ranchi hiyo kwa sasa imevamiwa na tembo zaidi ya 600 na wameharibu miundombinu na kuomba serikali kutoa msaada wa haraka kuwaondoa tembo hao.

Mwekezaji wa Ranchi ya Uvinza mkoani Kigoma, Benard Katamba, alisema wavamizi wamechukua maeneo yao, wanaiba mifugo yao jambo ambalo linawakatisha tamaa ya kuendelea na ufugaji.

"Sisi wawekezaji wa Ranchi ya Uvinza tumevamiwa haswa, mpaka sasa nimeshaibiwa ng'ombe 25 na mbuzi 150 na sina matumaini yoyote ya kuwapata, kwa kweli tunaomba msaada wa serikali," alisema.

Mwekezaji katika Ranchi ya Misenyi, mkoani Kagera, Nestory Lugakingira, alishauri serikali maeneo yaliyovamiwa yagaiwe kwa wavamizi ili sehemu itakayobaki itumiwe kwa ajili ya kuendeleza mifugo yao na kuepuka migogoro na wananchi hao.

Mwenyekiti wa Bodi ya NARCO, Paul Kimiti, aliiomba serikali kuangalia uwezekano wa NARCO kuwa na askari kama Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), ili kudhibiti hali hiyo.

Kufuatia ombi hilo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, aliwahakikishia kuwa serikali itachukua hatua kali kwa wale wote wanaovamia maeneo ya ranchi kinyume na sheria.

"Ninaelewa kwamba kuna maeneo ambayo wananchi wanakaa na kuwaondoa itakuwa ni uvunjifu wa haki za binadamu, maeneo hayo tutayaainisha na ili tuone kama tunataka kuendelea nayo au tukubali maeneo hayo yawe na matumizi mengine," alisema Ndaki.

# Sababu maambukizi ya VVU kwa wanawake hizi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MIONGONI mwa sababu zinazochangia maambukizi ya Virusi Vya UkimwiI (VVU) kwa wanawake na wasichana ni mila, desturi na ukatili wa kijinsia.

Kwa mujibu wa tathmini ya kitaifa juu ya mwitikio wa udhibiti wa VVU iliyofanywa na Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wanawake (UN-Women), mwaka 2018, inaonyesha asilimia 60 ya wanawake na wasichana wanaishi na VVU.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi, Fatuma Toufiq, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa katika warsha kwa viongozi wa kijamii, kisiasa, dini iliyoandaliwa na TACAIDS kwa kushirikiana na UN-Women.

Alisema utafiti umebaini kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya maambukizi ya VVU na ukatili wa kijinsia.

"Kwa kiasi kikubwa maambukizi ya VVU miongoni mwa wasichana na wanawake yanachangiwa na kutokuwapo na usawa katika mahusiano ya kijinsia na ukatili, ukatili wa kijinsia ni kichocheo cha maambukizi na madhara yanayotokana VVU," alisema.

Toufiq alisema baadhi ya wanawake na wasichana wamepata maambukizi ya VVU kutokana na ukatili wa kingono kwa kuwa hawawezi kuongea, hivyo kuingiliwa kimwili bila ridhaa.

"Mwanamke au msichana anapokwenda kukutana na mwenza wake hata hatamwambia kuwa tuchukue tahadhari hawezi kuongea mwisho wa siku anakuja kuwa ni mwathirika," alisema.

Hata hivyo, mwenyekiti huyo alisema wanawake wengi wenye VVU wako katika hatari ya ukatili pale wanapoweka wazi hali zao za maambukizi kwa jamii.

"Mwanamke akiweka wazi hali yake ya maambukizi anakumbana na unyanyapaa mkubwa kwa kuwa jamii inamwangalia kwa jicho tofauti wakati kwa mwanaume haionekani kwamba ni shida kubwa. Huu ni mfumo dume, tabia na mila na desturi inasababisha kukosekana kwa usawa wa kijinsia na ukatili wa kijinsia hapa Tanzania na inachochea na kuongeza maambukizi ya VVU," alisema.

Awali, Mkurugenzi katika idara ya inayoshughulika na Urakabishi na Habari wa TACAIDS, Jumanne Isango, alisema maambukizi ya VVU kwa kiasi kikubwa yapo kwa wanawake na wasichana na kuwataka viongozi hao kuweka mikakati ya kunusuru hali hiyo.

Mratibu wa Programu za Ukimwi na Jinsia UN-Women, Jacob Kayombo, alisema washiriki wa warsha hiyo watashiriki kuandaa mikakati kwa kushirikiana na TACAIDS ili kuondoa matatizo hayo.




Mdau wa zao la kahawa, mkoani Kagera, Shakiru Kyetema, akizungumza na Meneja wa Benki ya NBC tawi la Dodoma, Happiness Kizigira, wakati wa mkutano mkuu wa wadau wa zao hilo, mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. Benki hiyo ilikuwa moja ya wadhamini muhimu wa mkutano huo. MPIGAPICHA WETU

# Wahandisi watakaokula fedha za maji kwenda jela

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema mhandisi atakayekula fedha za maji ajiandae kwenda jela, huku akiwataka kuwa wazalendo katika utekelezaji wa miradi.

Aidha, amewaonya kuacha tabia ya uongo na kuwataka kuipa heshima taaluma yao kwa kutatua kero zinazowakabili wananchi.

Aweso alitoa kauli hiyo alipokuwa akifungua mafunzo kwa Mameneja wa Mikoa wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) ambayo yanalenga masuala ya kuzingatia maadili, kuepukana na vitendo vya rushwa kwenye majukumu yao.

"Wizara ya Maji haijaajiri vibaka imeajiri wataalamu wenye uwezo...Pesa ya maji ndugu zangu ukiamua kula pesa ya maji jela inakuita, twendeni tukafanye kazi."

"Hivi karibuni nitatoa mkeka sitamwonea mtu wala msiwe na wasiwasi nitawapa majukumu mazito mkafanye kazi, nimeona simu zimekuwa nyingi na wala hamna sababu ya kwenda kwa waganga kuliwa fedha zenu, katika kuleta ufanisi nitachanganya wahandisi nitatoa wengine wa RUWASA kwenda kwenye Mamlaka za Maji na wa Mamlaka nao watakuja wakala lengo ni kuleta ufanisi," alisema.

Aidha, alisema wahandisi hao wana uwezo wa kufanya kazi hivyo waende kufanya kazi na kama mtu hatafanya kazi atawekwa pembeni, na kwamba wajibu wao kila wakilala na kuamka ni kuhakikisha watu wanapata maji.

Aliwataka kufanya kazi na kuachana na visingizio visivyo na ulazima na kusisitiza kuwa kipimo kilichopo kwenye utendaji kazi wao ni kuona matokeo.

"Nilichokiona kwa wahandisi wa maji ni uongo, uongo, uongo, huwezi kuwa mhandisi wa maji muongo, unaitwa mtaalamu maana yake umesomea kitu kile unatakiwa kujibu kitaalamu lazima uheshimishe taaluma yako, kwa mfano juzi Mwanza mtu unamdanganya kiongozi wako haiwezekani kwasababu mimi ukiniambia kitu sikubaliani kirahisi, unasema watu wanateseka unaenda kwenye tangi maji yapo hadi juu."

"Unadanganya kwa faida ya nani? Lakini kama unaona wewe huwezi kufanya kazi kwa kasi hii hauwezi kwenda kwa mwenendo huu andika barua tutakusaidia, wala hatutagombana, andika barua kwamba kwa kipindi hichi naomba nipishe lakini hatutagombana na mtu tunataka tukatatue miradi ya maji," alisema.

Alisema fahari yao ni kuona wananchi wanapata maji, huku akiwataka viongozi hao kuzingatia mafunzo watakayopewa ili kuleta ufanisi na kujiepusha na vitendo vya rushwa.

Awali, Mkurugenzi wa Wakala huo, Mhandisi Clement Kivegalo, aliwaomba washiriki wa mafunzo hayo kuwa wasikivu kwa kuwa lengo ni kuwaongezea uwezo kwenye utendaji kazi na kufikia malengo yaliyowekwa ya kufikia asilimia 85 ya wananchi vijijini wawe wanapata maji.





# Fursa yaja wakulima kuuza mazao nje ya nchi

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI imeanza kufungua masoko ya mazao ya chakula nje ya mipaka ya nchi ili kuuza ziada iliyorundikana nchini bila soko.

Lengo ni kuwasaidia wakulima kupata bei nzuri ambayo itawawezesha kujikwamua kiuchumi na kuongeza tija katika kilimo.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, aliyasema hayo jana akiwa wilayani Mbarali, wakati akiwagawia wakulima zana bora za kilimo zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 950, ambazo ni mkopo uliotolewa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kwa wakulima.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameielekeza wizara yake kuanza kufungua masoko ya mazao ya wakulima nje ya mipaka ya Tanzania ikiwamo kutumia vema soko la Afrika Mashariki.

Alisema kwa kuanzia Rais mwenyewe alikwenda Kenya kwa ajili ya kufungua soko la nafaka za Tanzania nchini humo ambapo pia aliongozana na wafanyabiashara wa Tanzania pamoja na viongozi wa Wizara ya Kilimo.

"Rais wetu ameshatuagiza kufungua masoko ya mazao yetu nje ya mipaka ya Tanzania, kama mlivyoona yeye mwenyewe alikwenda Kenya na sasa mipaka ya kuuza mazao huko imeshafunguliwa na sisi kama wizara hivi karibuni tutakwenda Sudan ya Kusini kwa ajili ya mazungumzo mahususi ya kuuza huko nafaka zetu kama vile mchele na mahindi," alisema Prof. Mkenda.

Alisema mpango huo wa kufungua masoko ya mazao nje ya nchi pia umezilenga nchi za Zambia, Zimbabwe, Afrika Kusini na Jamhuri ya Kidemokasia ya Kongo (DRC).

Prof. Mkenda alisema kwa sasa Tanzania ina ziada ya mazao ya chakula zaidi ya tani milioni mbili ambazo bado zipo mikononi mwa wakulima.

Alisema kutokana na wakulima kuhifadhi mazao yao kwa muda mrefu bila kuyauza na kusababisha mavuno ya msimu mpya kukuta mazao ya msimu uliopita yakiwa ghalani bila kuuzwa, kimechangia mazao hayo kuuzwa kwa gharama ndogo.

Hata hivyo, aliwataka wakulima kuongeza tija kwenye kilimo ili waweze kupata mavuno mengi na bora kwa lengo la mazao yao kufanya vizuri sokoni ikiwa ni pamoja na kukidhi mahitaji ya wateja wao.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wa kilimo wataendelea kuwawezesha wakulima kwa kuwawekea mazingira mazuri ya kufanya shughuli zao ili waendelee kuzalisha kwa tija.

Awali akizungumza kwa niaba ya wananchi, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune alisema kukosekana kwa soko la uhakika la mazao ya wakulima kumechangia wakulima wengi kushindwa kumudu gharama za kilimo katika msimu unaofuata kutokana na kutokuwa na rasilimali fedha.

Alisema upatikanaji wa soko la uhakika la mazo ya wakulima utajibu kero nyingi za wakulima ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa zana bora za kilimo, pembejeo na gharama za kupeleka mazao yao sokoni.

Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alisema benki yake imeamua kuwawezesha wakulima kufanya shughuli zao kwa tija kwa kuwakopesha zana bora za kilimo na fedha kwa ajili ya kununulia pembejeo zilizo bora zaidi.

Alisema kwa kipindi cha miaka minne iliyopita benki hiyo ilishatoa mikopo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 32 kwa wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Alisema fedha hizo zilikopeshwa kwa vikundi vya wakulima kwa ajili ya kununulia pembejeo na zana bora za kilimo kwa lengo la kuongeza tija kwenye sekta ya kilimo. Justine alisema ili kumwinua mkulima, benki hiyo imeshusha kiwango cha riba ya mikopo yake kutoka asilimia 20 za awali ambapo kwa sasa mikopo hiyo inatozwa riba ya kati ya asilimia tisa na 13 kulingana na aina ya mkopo unaochukuliwa.



Diwani wa Kata ya Ilomba jijini Mbeya, Tonebo Chaula, akiwahutubia wananchi wa kata hiyo wakati wa ziara ya maofisa wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Mbeya (Mbeya-WSSA) ya kusikiliza kero za maji zinazowakabili wananchi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC atoa mwezi kuboreshwa Soko la Mwanjelwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ametoa siku 30 kwa maofisa wa idara ya mipango katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuandaa mkakati wa kuliboresha Soko la Kimataifa la Mwanjelwa ili kuongeza ukusanyaji wa mapato.

Homera alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha Baraza maalumu la Madiwani wa Halmashauri hiyo cha kujadili na kujibu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema soko hilo lilijengwa kwa fedha nyingi ambazo zilikopwa kutoka katika moja ya benki, lakini bado halina ufanisi kutokana na wafanyabiashara kuyakimbia baadhi ya maeneo ya soko hilo kutokana na kutokuwa na wateja.

Alisema maofisa mipango wa halmashauri hiyo ndio wanaotakiwa kuwashauri madiwani wa Jiji hilo namna ya kuboresha soko hilo, lakini mpaka sasa hawajafanya kazi hiyo na hivyo kuifanya serikali kukosa mapato.

"Hili soko nilianza kulisikia siku nyingi sana, lakini mpaka sasa halileti faida na nyie maofisa mipango mpo, sasa mnapanga mipango gani? Msipotekeleza agizo hili ndani ya mwezi mmoja niliowapa nitafanya maamuzi maana nyie wote mpo ndani ya mamlaka yangu," alisema Homera.

Alitishia kuwahamisha watendaji hao katika Jiji hilo na kuwapeleka katika halmashauri zingine za mkoa huo na kuwapeleka wengine ili wafanye kazi kwa ufasaha tofauti na ilivyo sasa hivi.

Aliwataka watendaji wa serikali hasa wakuu wa idara za halmashauri kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria ili kufikia azma ya serikali ya kuwahudumia wananchi.

Kwa upande wake Meya wa Jiji la Mbeya, Dormohamed Issa, alisema wafanyabiashara wamekuwa wakiyakimbia baadhi ya maeneo ya soko hilo hasa ghorofa ya juu kutokana na wateja kutoyafikia kirahisi.

Alisema hali hiyo imeifanya halmashauri hiyo kufikiria kulibadilisha eneo la juu na kulifanya kuwa ni ukumbi wa mikutano ambao utakuwa unakodiwa ili kuongeza ukusanyaji wa mapato na kuwa na uwezo wa kurejesha mkopo benki.

Alisema awali waliwahi kujenga vibanda vya biashara kuzunguka soko hilo, lakini aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya wakati huo, Albert Chalamila, aliamuru viondolewe kwa madai kuwa vilikuwa vinachafua taswira ya soko hilo.

Alisema kwa sasa wanafikiria pia kurejesha vibanda hivyo ili vipangishwe hasa kwa wafanyabiashara wadogo ili kuiongezea serikali uwezo wa kukusanya mapato.

"Eneo lote la juu tunataka tulifanye liwe ukumbi wa mikutano na eneo la kuzunguka soko hilo tunataka tujenge vibanda vilivyoondolewa awali maana tumebaini kwamba bado soko letu halituletei faida," alisema Issa.

Aidha, meya huyo alisema katika miaka ya karibuni Halmashauri ya Jiji hilo imekuwa ikipata hati safi, lakini hoja ya ujenzi wa soko hilo imekuwa vigumu kufutika kutokana na deni lililopo kuwa kubwa na kutolipika kwa haraka.

# Wazee wa Mbarali wawajia juu vijana

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

BAADHI ya wazee wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali wamelalamikia vitendo vya vijana wao, kuzaa watoto na kuwatelekezea.

Wamedai hali hiyo inawaletea mzigo wa kulea watoto hao huku wakiwa hawana uwezo kiuchumi.

Waliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ukatili dhidi ya Wazee ambayo katika wilaya hiyo yalifanyika katika Kata ya Mahongole yakiwa na kauli mbiu ya 'tupaze sauti kupinga ukatili kwa wazee'.

Akisoma risala kwa niaba ya wenzake Katibu wa Baraza la Wazee wilayani Mbarali, Michael Sanga, alisema kitendo cha kuwatelekezea watoto wao nyumbani na wao kwenda sehemu nyingine kutafuta maisha inawaongezea ugumu wa maisha.

Katika hatua nyingine, Sanga aliiomba serikali kutunga sheria itakayoziwezesha halmashauri nchini kutenga fedha kwa ajili ya kuwakopesha wazee ili wajikwamue kiuchumi kama inavyofanya kwenye makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Sanga alisema kumekuwa na dhana kuwa wazee hawana sifa ya kukopesheka kutokana na umri wao na kwamba mtazamo huo ni ukatili dhidi ya kundi hilo ambalo linapaswa kuwezeshwa kiuchumi.

Kwa upande wake mwenyekiti wa baraza la wazee katika halmashauri hiyo, Hezron Kapwela aliwataka vijana kuacha tabia ya kuuza mashamba yao kwani huo ndio urithi wao kwa sasa na miaka ijayo.

Aliwataja vijana wanaouza mashamba kuwa wamepitwa na wakati na kuwataka kuiga mfano wa wazee wao kwani nao wangeyauza enzi za ujana wao watoto wao wasingeyakuta.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema kitendo cha vijana kuwatelekeza watoto wao kwa wazazi kunachangia wimbi la umaskini na kuwasihi kujipanga vyema kabla ya kuzaa ili waweze kuwatunza badala ya kuwapa mzigo wazee.

Mfune ambaye aliwakilishwa na mkuu wa idara ya mazingira katika halmashauri hiyo, Raphael Shitindi, alisema pamoja na mambo mengine ataziwasilisha changamoto za wazee hao ngazi za juu kwa ajili ya kushughulikiwa.



## Benki ya NMB yakaribishwa uchumi bluu Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imeipokea kwa mikono miwili Benki ya NMB katika kuhakikisha inapeleka mbele mikakati ya kufikia uchumi wa bluu hasa katika kukuza utalii.

Hayo yalielezwa na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Abllah Suleiman Abdallah, alipomwakilisha Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kwenye uzinduzi wa umoja wa wamiliki wa hoteli (HAZ).

Alisema, kitendo walichokionyesha Benki ya NMB kuwa mdhamini mkuu wa hafla ya uzinduzi wa HAZ kinadhihirisha dhamira ya dhati waliyokuwa nayo katika kukuza utalii visiwani Zanzibar, bila kujali hali ya sasa ya kuenea kwa ugonjwa wa Covid-19.

"Tunaipokea Benki ya NMB kwa mikono miwili visiwani Zanzibar, uwekezaji wa hoteli unazidi kukua na hamkukosea kulenga sekta hii ya hoteli. Idadi ya hoteli inakua kwa kasi Zanzibar ambapo mwaka 2018 zilikuwapo hoteli 509, na sasa zimefikia 620, yaani kwa mwaka zinaongezeka hoteli kati ya 25 hadi 36," alisema Abdallah.

Alisema ili serikali itimize malengo yake, inategemea kwa kiasi kikubwa wawekezaji, ndiyo maana wameamua kufungua milango ili wawekezaji wa ndani na nje wapate fursa za kukuza biashara na kuanzia biashara mpya.

Naye Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, alisema biashara ya hoteli inachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa Zanzibar, hivyo anaamini fursa ni kubwa hasa ikizingatiwa zaidi ya hoteli 500 zilizopo ikiwa ni sawa na zaidi ya vitanda 900, Zanzibar inaweza kupokea wageni wengi ikiwa kutakuwa na ubunifu wa kutosha.

"Tumesikia pia kilio chenu wamiliki wa hoteli juu ya majanga ya moto na changamoto ya kutopata fidia kwa wakati, tunawahakikishia kuwa utaratibu wetu wa bima ni wa kipekee na unamhakikishia mteja kupata fidia yake yote kwa wakati."

Katika hatua nyingine, Mponzi alisema Benki ya NMB imefungua fursa pana kwa Zanzibar, kwa sasa kuna ATM 17 ambapo zipo nyingine saba zinaongezwa katika maeneo mbalimbali ikiwamo ATM inayotoa huduma ya kubadilisha fedha za kigeni itakayowekwa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume uliomalizika kujengwa hivi karibuni.

# Jamii yahimizwa kuwalinda watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, amewataka wazazi na walezi kubadili mitazamo ya maisha kwa kutowaamini watu wasiowajua, kwa lengo la kuwaepusha watoto wao dhidi ya majanga mbalimbali yakiwamo ya udhalilishaji wa kijinsia.

Aliyasema hayo jana mjini Unguja katika maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika yalioadhimishwa na taasisi mbalimbali zisizokuwa za kiserikali.

Alisema licha ya uwapo wa matatizo hayo hatarishi kwa watoto, lakini hadi leo wapo baadhi ya wazazi kwenye familia hawana utaratibu wa kuwalinda watoto wao wala kuwafuatilia nyendo zao na ndio maana wati kadhaa hutumia mwanya huo kuwafanyia maovu watoto wadogo.

Alisema wazazi wana wajibu wa kuwaeleza watoto wao kukataa kuitikia wito au hata kupanda kwenye chombo chochote cha usafiri kutoka cha mtu wasiyemjua.

"Hivi karibuni tu tumepokea taarifa kuwa kuna mtoto aliyefanyiwa udhalilishaji na mtu aliyempakia kwenye pikipiki, mtu huyo awali alimuita mtoto huyo na kumpakiza kisha kumpeleka anapotaka yeye, lakini kwa bahati nzuri raia wema walimwokoa mtoto huyo hatimaye mhusika kudhibitiwa," alisema Dk. Mzuri.

Katika hatua nyingine, mkurugenzi huyo alizitaka mamlaka zinazojihusisha na kesi za udhalilishaji kutotumia kigezo cha ushahidi wa mtoto anaposema aliyemfanyia kitendo cha kumdhalilisha kimaumbile ni mpenzi wake kwa kuwa msichana huyo hajatimiza umri wa miaka 18.

Alisema kikawaida msichana asiyetimiza umri wa miaka 18 hata kama amejaliwa maumbile makubwa, haweza kufanya kitu bila ya kushawishiwa na mwanaume na inapotokea amefanya na kukiri kuwa kafanya kwa ridhaa yake mahakimu hawapaswi kuchukua kauli hiyo kama sehemu ya kumwachia mtuhumiwa wa udhalilishaji.

Akisoma risala kwa niaba ya watoto wenzake, Salma Abeid, alisema licha ya kuwapo Siku ya Mtoto wa Afrika bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali.

Akitaja changamoto hizo ni uwepo wa ndoa za umri mdogo na kulazimishwa kazi zisizolingana na umri hatimaye kuwadumaza kiakili.

Pia alisema suala la udhalilishaji wa kijinsia ni jambo linalowapa wakati mgumu watoto wengi na wapo waliofanyiwa matendo hayo kubaki na kusononeka daima, huku wakishindwa hata kurudi shule.

Alieleza kuwa wao kama watoto wa Afrika wana ndoto nyingi zinazohitaji kuendelezwa kutoka kwa wazazi wao na jamii kwa ujumla.

Awali akisoma ripoti ya utafiti mdogo uliofanywa na TAMWA, Meneja miradi wa chama hicho, Ally Mhamed, alisema utafiti huo umebaini uwapo wa kasoro mbalimbali katika vyombo vinavyojihusisha na mapambano katika kesi za udhalilishaji.

Alitolea mfano uhaba wa usafiri katika vituo vingi vya polisi Zanzibar ni tatizo linalosababisha maofisa wa jeshi hilo kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa haraka pale wanapopata taarifa za kutokea kwa matukio katika maeneo tofauti.

Kadhalika, alitaja uhaba wa vitendea kazi na sehemu za kusikiliza kesi za udhalilishaji katika mahakama mbalimbali visiwani Zanzibar na kusababisha mrundikano mkubwa wa kesi hizo katika mahakama.



Rais mstaafu wa Zanzibar, Amani Abeid Karume, akizungumza katika mkutano wa watumishi wa serikali waliostaafu ulioandaliwa na Benki ya CRDB ambao umefanyika ukumbi wa Kariakoo mjini Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ yaunda kamati mgogoro wa ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeunda kamati ya kufuatilia mgogoro wa ardhi kati ya wananchi na kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) katika kijiji cha Ubago Wilaya ya Kati Unguja.

Akizungumza na wananchi wa kijiji hicho, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadidi, alisema imeshaundwa kamati ya kufuatilia upimaji wa maeneo yote yenye migogoro ya ardhi katika mkoa huo kwa ajili ya kuyatafutia ufumbuzi.

Alisema Ofisi ya Mkoa kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi imeanza kuyakagua maeneo hayo ili kuangalia mipaka kwa ajili ya hatua ya upimaji.

Mkuu wa Mkoa huyo alieleza kuwa mgogoro wa ardhi uliopo katika mkoa huo unasababisha migongano kati ya wananchi na jeshi katika kambi ya Ubago na baadhi ya maeneo ya vijiji vya jirani, hivyo kusababisha uhasama katika jamii.

Hadidi aliwataka wananchi kuwa wastahimilivu wakati serikali inalishughulikia tatizo hilo na kulitafutia ufumbuzi ili jamii ipate kuishi kwa amani na ushirikiano na serikali.

"Ndugu zangu wananchi wa Ubago tutulieni na tuamini serikali ambayo ipo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi kwa kuwapa huduma bora ikiwamo kuwatatulia changamoto zinazowakabili."

Aliwasisitiza wakazi wa maeneo yenye migogoro kutoa ushirikiano kwa watendaji wa Wizara ya Ardhi watakapopita katika meneo yao kutoa maelezo ya kina ili kufanikisha zoezi hilo.

Mkuu huyo wa Mkoa alimtaka sheha wa Shehia ya Ubago kuunda kamati ya watu 12 watakaowakilisha wananchi kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kati, Marina Joel Thomas, aliwataka wananchi wa Ubago kuzitumia ofisi za wilaya kuyafikisha malalamiko kwa lengo la kupatiwa ufumbuzi na kuchukuliwa hatua husika.

Kwa upande wao wananchi wa Kijiji cha Ubago waliiomba serikali kuupatia ufumbuzi wa haraka mgogoro huo pamoja na kufanya mazungumzo na uongozi wa kambi ya jeshi ili kuwaruhusu kufanya shughuli zao za kilimo na uchimbaji.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## CLASSFIED-NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA IPO KIBAHA KWA MATIAS INAVYUMBA VINNE ,VIWILI MASTA,UMEME UPO,MAJI YAPO KARIBU MITA 30,BEI MILLIONI 45. KWA MAWASILIANO:0759 454092

116319302

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
SHAURI LA MIRATHI NAMBA 119 LA 2021
Maombi ya barua za usimamizi wa mirathi ya marehemu
DAMAS SIMELI MKAMI.........MAREHEMU
FLORIAN DAMAS MKAMI......MWOMBAJI
TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 30 mwezi 06 mwaka 2021

Hati hii imetolewa 21 mwezi 06 mwaka 2021

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

116319402

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.40 OF 2021
In the matter of the Estate of the late JOEL SIMON CHIBALUWA of Matumbulu within Dodoma City
And
In the matter of the application for letters of administration by GRACE SIMON CHIBALUWA
GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules GN 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 28 day of 07/2021.
**Dated at Dodoma this 21 day of 06/ 2021**

116319702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KUITWA SHAURINI
MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU
WILAYA YA GEITA
MADAI NAMBARI 89/2021
MDAI: ELIZABETH BARTHARI SHAYO
DHIDI YA
MDAIWA: LEILA HASHIFU**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai dhidi yako Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya tarehe 23/06/2021 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 14/06/2021

HAKIMU

116320002

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DAR ES SALAAM
UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI
MIRATHI Na. 60 YA MWAKA 2021
MAOMBI YA BARUZA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU
MTANGO JOTHAM LUKWARO
MWOMBAJI/WAOMBAJI
LUSIU ANDREW PETER
TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 5th Mwezi wa July, 2021.
Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 10th Mwezi wa June, 2021.

NAIBU MSAJILI

116319202

## NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED
## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

M/MWANZO MWANZA MJINI - SHAURI LA MADAI Na. 30/2020

MUSSA OMARY HASSAN________MDAI
DHIDI YA
DATUS SAFARI SHIRIWA________MDAIWA

M/ MWANZO KISESA - SHAURI LA MADAI Na. 33/2020

SINJA MASATU________MDAI
DHIDI YA
ESTA MAKOYE (LUSIA SOMI)________MDAIWA

M/ MWANZO KISESA - SHAURI LA MADAI Na. 35/2020

SIMON CHASAMA (MWENYEKITI WA UALBINO BUJORA)_
MDAI
DHIDI YA
LUSIA SOMI ________MDAIWA

M/MWANZO BUKUMBI - SHAURI LA MADAI Na. 10/2020

DIANA IBRAHIM________MDAI
DHIDI YA
SIMON JOHN________MDAIWA

M/ MWANZO MWANZA MJINI - SHAURI LA JINAI Na. 752/2020

KAZIMILI PAUL________MDAI
DHIDI YA
MICHAEL MWENDAGWAZA MAYALA________MDAIWA

KWA IDHINI NA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO MWANZA MJINI, BUKUMBI NA KISESA TUNAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA WADAAWA. MNADA UTAFANYIKA MAHALA MALI ILIPO.

| SN | MALI INAYOUZWA | MAHALI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | NYUMBA | NYUMBA NAMBA 799 KITALU "FF" ILIYOKO MTAA WA MECCO KUSINI NYAMAGANA | 27/7/2021 SAA 3 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | NYUMBA | NYUMBA YENYE VYUMBA VIWILI NA SEBULE ILIYOPO NG'WANDULU MTAA WA JOSEPH JOHN | 27/7/2021 SAA 5 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3 | NYUMBA | ILIYOKO KWENYE KIWANJA NAMBA 321 KITALU "A" KATIKA ENEO LA MBUGANI- NDOFE | 28/7/2021 SAA 3 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 4 | NYUMBA | ILIYOPO KITONGOJI CHA MTAKUJA KATA YA USAGARA WILAYA YA MISUNGWI | 28/7/2021 SAA 5 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA:**
1. MTEJA ATALIPA ASILIMIA ISHIRINI NA TANO YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA ITAKAYOSALIA ATALIPA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE. KUSHINDWA KUFANYA HIVYO MTEJA ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI YAKE YA MSINGI NA MNADA UTARUDIWA TENA.
2. GHARAMA ZOTE ZITAKAZOJITOKEZA BAADA YA KUNUNUA MALI KWENYE MNADA NI JUU YA MNUNUZI.

**MAWASILIANO: 0768-588155.**

116319902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SAIDI RASHID KAMBI** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 439 DPE – TOYOTA IST.** CHASSIS NAMBA **NCP600211043.** ENGINE NAMBA **2NZ3590558.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/MBA/RB/304616/2021.**

116319802

## KUPOTEA KWA CHETI



**AWADH MOHAMED CHICO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0469/340** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia Shule ya Secondari JITEGEMEE mwaka 1996. Yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/URA/RB/309489/2021**

116320102

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD,** dalali tajwa hapo chini tutauza kwa mnada wa hadhara Mali za wadaiwa Sugu kama ilivyotangazwa kwenye gazeti/;-

| Mdaiwa/ mdhamini | Dalali | Aina ya Mali | Tarehe ya mnada - Mahali |
|---|---|---|---|
| ESTHER AMIR ABUSHEE | **TAUSI** AUCTION MART | Nyumba | 16/07/2021- Goba - Kunguru |
| Haji Jamadin Chitonya/ Franklin.Mlay | **TAUSI** AUCTION MART | Nyumba | 12/07/2021 Buza- Mwinyi road |

Minada yote itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:
TAUSI - 0719351040/0713237650**

116320202

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MBEYA
SHAURI LA RUFAA YA JINAI NO. 38/2019
(EXTENDED "J")
(Kutoka Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya,jinai No.68/2017)
JAMHURI..............................MUOMBA RUFAA
DHIDI YA
ELIAS KAYOWA........................MJIBU RUFAA
KWA :
BWANA: ELIAS KAYOWA
POPOTE ULIPO -TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI**
Unaamuriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya Tarehe 24/06/2021 siku ya Jumatano saa 03.00 asubuhi bila kukosa.
ELEWA KWAMBA,ukikosa siku hiyo, Shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25/5/2021.

**Z.D.Laizer
HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MBEYA**

26316802

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

## Tanzania kukaribisha wawekezaji ndani na nje

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Profesa Kitila Mkumbo, amesema ili Tanzania kufikia dira ya maendeleo kama ilivyokusudiwa, wanatarajia kukaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi katika maeneo muhimu ya kiuchumi ikiwamo Kurasini jijini Dar es Salaam.

Prof. Mkumbo aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ufunguzi wa kongamano lililolenga kujadili uhusiano baina ya maeneo maalum ya uwekezaji na uchumi wa ndani lililoandaliwa na Taasisi ya Uongozi Institute na Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Mauzo ya Nje (EPZA).

Alisema ili Tanzania kuwa ni nchi ya viwanda na uchumi endelevu wameweka mkazo mkubwa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda katika mitaa kwa maeneo mbalimbali muhimu nchini.

Alisema maeneo mengine ambayo yanatarajiwa kutengenezwa mitaa ya viwanda ikiachwa Kurasini ni mkoa wa Arusha, Mwanza na Pwani (Bagamoyo) na tayari maeneo yameshatambuliwa na mikakati ya kuyaendeleza yanafanyika.

Prof. Mkumbo alisema katika eneo la Kurasani hivi karibuni tangazo litatoka na wanatarajia kupata maombi mengi kwa ajili ya uwekezaji wa ndani na wa kimataifa.

"Tunataka tushindanishe ili tupate mwekezaji mzuri kwa ajili ya kuwekeza katika eneo la Kurasini kwa kuwa limekaa muda mrefu, serikali imekusudia kutengeneza mitaa ya viwanda kwa baadhi ya mikoa," alisema.

"Tunawakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuchangamkia eneo la Kurasini ambalo litakuwa wazi kwa kutangazwa baadaye mwaka huu na tumekubaliana tangazo litatoka nadhani ni Julai au Agosti mwaka huu ili tushindanishe tumpate mwekezaji mzuri ili serikali liweze kuendeleza hilo eneo," alisema.

Pia, alisema katika maeneo maalum ya kiuchumi wawekezaji wameanza kujitokeza kwa wingi na kwamba hakuna vikwazo kwa kuwa rais amesisitiza kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji.

Aliitaka EPZA kuhakikisha shughuli wanazozifanya zinafahamika na wananchi wa kawaida pamoja na wadau.

Alisema hata Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alivyotembelea EPZA alizungumza umuhimu wa kuongeza kasi ya kutangaza habari za EPZA na shughuli zake.

Alisema lengo kubwa ni kujenga uelewa wa EPZA na fursa zilizopo ili iweze kufahamika na wadau kufanya uwekezaji.



Mkufunzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Somoye Mkwacho, akiwapa maelekezo baadhi ya wanafunzi kutoka shule mbalimbali za sekondari zilizoko Kanda ya Ziwa wakati wa mafunzo ya TEHAMA yaliyopewa jina la 'Code like a girl', mpango ulioanzishwa na Vodacom Tanzania chini ya Taasisi isiyo ya Kiserikali ya D Lab ili kutoa hamasa kwa wasichana waweze kupenda masomo ya sayansi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mdee ashtukia upigaji stempu za kielektroniki

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum, Halima Mdee, ameitaka serikali kuja na majibu ni lini itavunja mkataba wa uwekaji wa stempu za kielektroniki kwenye bidhaa mbalimbali, kati yake na Kampuni ya Societe Industrielle de Produits Alimentaire (SICPA) ya Uswisi, yenye ubia na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Ametaka kandarasi hiyo kuondolewa na kurudishwa serikalini au ufanyike ushindani, watu waje na apatikane mtu mwenye gharama nafuu, badala ya kuendelea kupigwa katika mkataba huo.

Mdee alikuwa akichangia jana mjadala huo bungeni, kuhusu hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2020 na mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka wa fedha 2021/22 na makadirio ya mapato na manunuzi ya serikali kwa mwaka wa fedha 2021/22.

"Sasa hivi ninaitaka serikali na Waziri Mwigulu ananisikiliza. Nataka Mheshimiwa Mwigulu, hili la ETS (mfumo wa stempu za kielektroniki) ulitoe huko kwa mkandarasi aliyeko sasa, kwa sababu tumeshapigwa vya kutosha, turudishe ama serikalini kama serikali haina teknolojia, tufanye ushindani, watu waje tupate mtu mwenye gharama nafuu.

"Mheshimiwa Mwigulu, nitakuomba tu unijibu, kiukweli tunapigwapigwa sana na si busara kukubali kuendelea kupigwapigwa, na mimi najua wewe hupendi kupigwapigwa."

Wakati anaanza kuchangia, Mdee alimtaka Waziri Mwigulu atakapojibu hoja za wabunge, aeleze ni kwa namna gani stika hizo ambazo zinatokana na mikataba mibovu na ya ovyo, zilisababisha mkandarasi binafsi kwa mwaka kupata zaidi ya Sh. bilioni 68, kwa miaka minane aliyekuwapo kupata Sh. bilioni 490.

"Nataka uniambie, mkandarasi huyu huyu ambaye amepewa jukumu la kubandika stempu za kielektroniki ama ETS kwenye bidhaa zinazozalishwa nchini kwa ajili ya kutoza ushuru wa bidhaa, mkataba wake utakoma lini ili hili jukumu ambalo amepewa mkandarasi huyu, kipewe ama chombo cha serikali, ama mfanye ushindani huru na apatikane mkandarasi wa bei nafuu.

"Tuzungumze juu ya mafuta na nitazungumza juu ya ETS. Kwa maelezo ya serikali, huu utaratibu ulianza mwaka 2018, kwa wanaofikiria kipindi kile mambo yalikuwa perfect sana (yalikuwa yanaenda vizuri), lakini sio kila kitu ni perfect.

"Tunasema haya lazima tujirekebishe. Lengo lake lilikuwa ni jema kutambua bidhaa, kuzuia watu wasikwepe kodi, serikali ipate kodi yake stahiki, lakini gharama tunaambiwa mpaka sasa hivi wazalishaji ambao wamefungiwa hizo mashine wako 245 na waagizaji 86.

Sasa mafanikio ni nini? Kwa Petroli ilikuwa ukiweka pale bei ya lita moja ni shilingi nane, huku kwenye bidhaa za vinywaji vikali na vyepesi, sigara na kadhalika, kuna shilingi nane kwa mantiki ya dola nane na dola 20 kutegemeana. Sasa mafanikio ni nini, kabla ya ETS na baada ya ETS.

"Kwa maelezo ya TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania), kabla ya ETS tulikuwa tunakusanya shilingi bilioni 237, baada ya ETS, tumekusanya shilingi bilioni 246. Tafsiri yake ni nini? Tofauti nyie mnajua, bilioni 46 toa bilioni 37 ni bilioni nane.

Aidha, Mdee, alifafanua zaidi akisema, gharama ambazo kampuni zinaingia kutokana na huu mchakato ni mengi na kwamba taarifa ya Kampuni ya Bia (TBL), ambayo ni walipakodi wakubwa nchini, inasema katika kipindi cha miaka mitatu, wanatarajia kuanzia 2019 hadi 2021 watamlipa mkandarasi Sh. bilioni 94.

Vilevile, kampuni ama viwanda vilivyounganishwa ni zaidi ya 250, wakati TRA nyongeza yao ni kupata Sh. bilioni 237 mpaka Sh. bilioni 256, tofauti ya Sh. bilioni nane.

"TRA wakatupa data zao za ndani (takwimu) kwamba kabla ya mtambo wa ETS, shilingi milioni 657, baada ya ETS on average (kwa wastani) iliongezeka mpaka Sh. bilioni 3.4

"Mmefanya na TBL hapo, mkandarasi binafsi kalipwa na TBL bilioni zaidi ya 90. Kwenye hilo serikali ili ijue kuna cheating kubwa (danganyifu), mnapata bilioni nane, hivi tukisema hii ni busara?

Baada ya Mdee kuhoji hilo, Mbunge wa Bahi (CCM), Keneth Nolo, aliomba kumpa taarifa Mdee akisema, "Mheshimiwa Naibu Spika (Dk. Tulia Ackson), nataka nimpe taarifa mzungumzaji, nadhani anajaribu kutoa opinion (mawazo) tangu kule alikosema kwenye mafuta na hata huku.

Na kitendo cha kutamka kampuni hii inalipa kiasi hiki cha fedha ni kama anataka kusema kuna uonevu. Kwa hiyo hoja yake ya msingi hapa angejaribu kusema kwamba altenative (njia mbadala) ni tutafute kampuni nyingine. Tunapotaja kwamba hawa wanalipa kiasi hiki, ni kama watu wanaonewa.

Alipomaliza kutoa taarifa hiyo, Mdee alisema anachokizungumza hakina tofauti na alichokizungumza Hamisi Tabasam (Mbunge wa Sengerema) kuhusiana na mfumo huo kwenye mafuta.

Kauli hiyo ikamwinua tena, Mbunge wa Maswa Mashariki (CCM), Stanslaus Nyongo ambaye alimweleza Mdee kwamba yeye mwenyewe ni mjumbe wa kamati ya bajeti, na hayo yote yamepita kwenye kamati ya bajeti na jambo jingine, suala la ETS liliibuliwa kwenye kamati ya bajeti na serikali imekuwa ikisimamia na kupambana na suala hilo kuhakikisha kwamba linakuwa na faida.




# BALE
## NINA UHAKIKA KURUDI REAL MADRID

**ROME, Italia**

GARETH Bale ameeleza kwamba, yupo tayari kurejea Real Madrid wakati huu wa majira ya joto, na amemsifu kocha mpya, Carlo Ancelotti na kusema kuwa ana mahusiano makubwa na raia huyo wa Italia.

Ingawa hatima ya Bale baada ya Euro 2020 bado haina uhakika, kurejea kwa Ancelotti kunamfanya mshambuliaji huyo wa Wales kuonekana ni kama atarejea Real Madrid baada ya kucheza kwa mkopo kule Tottenhma Hotspur kwa msimu mmoja.

"Naweza kusema kuwa nina mahusiano mazuri na yeye Carlo Ancelotti," alisema Bale katika mkutano wake na waandishi wa habari kabla ya mchezo wa Wales dhidi ya Italia, Jumapili.

"Ni kocha mkubwa na ameshafanya mambo makubwa Real Madrid na sasa amerudi tena."

Bale aliongeza kusema kwamba, kwa sasa ana uhakika mkubwa wa kurudi pale Santiago Barnabeu kwenda kupambania namba yake ambapo alikuwa hana nafasi chini ya Zinedine Zidane.

Bale amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake na Real Madrid na angependa kurudi kumalizia kipindi chake kilichobaki."

## ARSENAL YATOA OFA YA PILI KWA CORREA

**LONDON, England**

ARSENAL wameripotiwa kuwasiliana na Lazio wakiwa na ofa iliyoboreshwa kwa ajili ya nyota, Joaquin Correa.

Arsenal wanawania kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 na hivi karibuni waliwasilisha ofa ya Euro milioni 20, lakini Lazio waliikataa.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Il Messaggero, Arsenal sasa wamewasilisha ofa kati ya Euro milioni 15 na milioni 20 kwa ajili ya Correa.

Pia Arsenal ipo tayari kumtoa Lucas Torreira kama sehemu ya makubaliano hayo na upande wa miamba hao wa Serie A.

Taarifa zinadai kwamba Lazio wako tayari kukubali pendekezo la sasa, na Correa ana matumaini kuwa uhamisho wa kwenda kule dimba la Emirates unaweza kukubaliwa katika siku za usoni.

Raia huyo wa Argentina, ambaye amekuwa pia akihusishwa na Liverpool, alifunga mabao 11 na kusajili pasi za mwisho sita katika mechi 38 klabuni hapo wakati wa kampeni ya msimu wa 2020-21.

Wakati huo huo, mshambuliaji huyo amepachika mabao 30 na kuchangia pasi za mwisho 18 katika mechi 117 za Lazio tangu ajiunge nayo kutoka Sevilla mwaka 2018.



# CHELSEA YAFUNGUA MAZUNGUMZO NA KANTE

**LONDON, England**

CHELSEA inaripotiwa kuanza mazungumzo na nyota wao N'Golo Kante juu ya mkataba mpya katika miezi ijayo.


Hatima ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 30 huko Stamford Bridge, ilianza kuwa katika sintofahamu msimu wa joto uliopita, lakini mwishowe alibaki na Chelsea na kufanikiwa kufanya vema huko, akicheza mechi 48 katika mashindano yote msimu wa 2020-21.

Kante amebakiza miaka miwili tu katika mkataba wake wa sasa na kwa mujibu wa chanzo kimoja cha habari cha nchini Italia, Chelsea wanapanga kufungua mazungumzo ya mkataba mpya na mshindi huyu wa Kombe la Dunia katika miezi michache ijayo.

Taarifa zinadai kwamba kulikuwa na ofa mbili kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa wakati wa usajili wa msimu uliopita wa kiangazi, lakini alitaka kubaki klabuni hapo.

Sasa Chelsea wanadaiwa kuwa wanataka kumzawadia N'Golo Kante, ambaye kwa sasa anaiwakilisha nchi yake kwenye mashindano ya kimataifa ya Euro 2020.


Kante amecheza mechi 218 kwa 'Blues' hao tangu alipowasili kutoka Leicester City mwaka 2016.





# MANCINI: ITALIA IMEBAKIZA MECHI NGUMU EURO 2020

**ROME, Italia**




KIKOSI cha Italia kinafahamu kwamba, kinakabiliwa na kazi tofauti wakati huu kikiwa kimeshatinga hatua ya mtoano ya michuano ya Euro 2020, amesema Roberto Mancini.

'Azzurri' hao waliweka rekodi ya kushinda kwa asilimia 100 hatua ya makundi ya michuano hiyo baada ya juzi kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Wales.

Bao la ushindi lilifungwa na Matteo Pessina kipindi cha kwanza, huku Wales wakimpoteza Ethan Ampadu kwa kadi nyekundu.

Ushindi huo uliwafanya Italia kufikisha mechi 30 bila kupoteza kwenye mashindano yote (wakishinda 5, sare 5) tangu walipopoteza kwa Ureno Septemba 2018, na kuweka rekodi ya kutopoteza mechi nyingi zaidi katika historia yao ambayo waliiweka kwa mara ya kwanza kati ya mwaka 1935 na 1939.

Kikosi hicho cha Mancini kimeshinda mechi zake 11 zilizopita na kutoruhusu nyavu zao kutikiswa.

Wapo kileleni kwenye Kundi A, Italia watacheza kati ya Ukraine au Austria kule Wembley kwenye hatua ya 16 Jumamosi inayokuja na Mancini anajua kazi iliyopo mbele yao.

Mancini aliiambia ITV Sport: "Tuna furaha, lakini tunajua kazi iliyopo mbele yetu ni tofauti. Na sasa tunajua kazi kubwa iliyopo mbele yetu.

"Nina uhakika kwamba, hatua hii ni ngumu, lakini lazima tutatakiwa kuwa makini na hivyo lazima tuwe tofauti."

# SOUTHGATE AKATA TAMAA UBINGWA ENGLAND EURO

**LONDON, England**

KOCHA wa timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate, amedai kuwa timu yake kwa sasa bado ipo kwenye kutengeneza kikosi kama ilivyo kwa timu nyingine, hivyo mashabiki wanatakiwa kuwa na subira.

Katika mahojiano na waandishi wa habari, baada ya kuulizwa kuhusu kama England itabeba Kombe la Euro 2020, Southgate alisema: "Nadhani nimewajibu hilo swali mara nyingi sana, watazameni Italia wana zaidi ya mechi 29 hawajapoteza.

"Watazameni Ureno na Ufaransa mambo waliyofanya miaka kadhaa nyuma, itazame Ubelgiji imekuwa namba moja duniani kwa miaka minne.

"Hilo ndio daraja tunalopaswa kufika, sisi England bado hatujafikia huko, sisi bado tunajijenga upya."

Mashabiki wengi wa England wamekuwa wakipinga maamuzi ya kocha Southgate kutokana na upangaji wa kikosi na mbinu ambazo zinaonekana hazina mashiko.

England leo Jumanne itacheza mchezo wake wa mwisho wa Kundi D dhidi ya Jamhuri ya Czech.

Kwa sasa England ina pointi nne baada ya kushinda mchezo wa kwanza dhidi ya Croatia na baadaye kutoka suluhu na Scotland.




# HAZARD AANZA KUHISI UZEE

**ST PETERBURG, Russia**

EDEN Hazard amesema kamwe hawezi kuwa kwenye ubora sawa kama ilivyokuwa miaka 10 iliyopita, hasa wakati huu akiwakilisha Ubelgiji kwenye michuano ya Euro 2020.

Kocha wa Ubelgiji, Roberto Martinez alimtumia kwa mara ya kwanza Hazard akitokea benchi wakati kikosi hicho kikiibuka na ushindi kwenye mechi mbili za Kundi B dhidi ya Russia na kisha Denmark.

Hazard mwenye umri wa miaka 30, ambaye anakipiga kule Real Madrid, amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara tangu atue kwa miamba hao wa dimba la Santiago Barnabeu.

Kwa msimu wa 2020-21, Hazard amecheza dakika 896 katika mashindano yote, akiwa amecheza jumla ya mechi 21.

Katika mechi zote hizo, alianza mara 11 tu, huku Hazard akifunga mabao manne na pasi za mwisho mbili na kutengeneza nafasi 10.


Nyota huyo wa zamani wa Chelsea amesisitiza bado yuko fiti na uwezo wa kuonyesha ubora wake, ingawa si kwa kiwango kama cha zamani.

"Kamwe sijawahi kuhofia kiwango changu, lakini hata kama nikiwa fiti kwa asilimia 100 kwenye michuano hii ya Ulaya, bado kutakuwa na maswali," alisema Hazard akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa mwisho wa kundi jana Jumatatu dhidi ya Finland.

"Nilivunjika kifundo cha mguu mara tatu, kamwe siwezi kuwa sawa kama ilivyokuwa miaka 10 iliyopita.

"Lakini najua kwamba, wakati nikiwa fiti naweza kucheza kwa kiwango bora, lakini sio kama zamani."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA SASA KULIPWA ZAIDI LIGI KUU ENGLAND

●●● Lengo ni kuzizuia Juve na PSG kumshawishi kuondoka wakati huu mkataba wake...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United ipo tayari kumpa ofa mpya, Paul Pogba ambayo itamfanya kuwa mchezaji anayelipwa zaidi kwenye Ligi Kuu ya England (EPL), kwa mujibu wa The Sun.

Majaliwa ya Pogba bado hayajulikani pale Man United huku akiwa amebakiwa na miezi 12 katika mkataba wake wa sasa.

Huku kukiwa na uvumi mwingi kuhusu Pogba na ripoti nyingine zikisema kwamba, amekuwa anaangalia uwezekano wa kuondoka hapo Old Trafford, sasa 'Mashetani Wekundu' hao wanapanga kumbakiza.

**Pogba raia wa Ufaransa, amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi Juventus ya Italia kipindi hiki cha majira ya joto.**

Juventus wameripotiwa kwamba, wanaitaka tena huduma ya mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa mwaka 2018, ambapo aling'ara pale Turin kabla ya kurudi Man United, ambapo alihudumu akiwa kinda.

Licha ya Juventus kutajwa kumwania, lakini miamba ya soka la Ufaransa, Paris St-Germain nao wamekuwa kwenye rada za kuwania saini ya Pogba mwenye umri wa miaka 28.

Na sasa Man United imeweka wazi kwamba inapanga kumpa dili lenye thamani ya pauni milioni 104.

Ripoti hiyo inasema kwamba, Man United inajiandaa kumpa ofa ya mshahara wa pauni 400,000 kwa wiki na mkataba wa miaka mitano kuendelea kukaa hapo Old Trafford.

Kwa mujibu wa gazeti la The Sun, Man United watampa ofa hiyo baada ya michuano ya Euro 2020 inayoendelea hivi sasa na Pogba akiwa na kikosi cha Ufaransa.

## KWA UFUPI

**UTD YATAJIWA BEI YA SANCHO**

BORUSSIA Dortmund imeitajia Manchester United bei ya mwisho ya paundi milioni 77 na marupurupu mengine kumsaini winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 21. (***Talksport***)

**PSG BADO YAMTAKA VARANE**

KLABU ya Paris St-Germain imewasiliana na Real Madrid kuhusu uwezekano wa kumsajili mlinzi wa Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 28. (***Foot Mercato***)

**ARSENAL YAMWANIA SILVA**

ARSENAL wameanza mazungumzo na Eintracht Frankfurt kuhusu uhamisho wa mshambuliaji wa Ureno, Andre Silva mwenye umri wa miaka 25, ambaye anauzwa kwa karibu pauni milioni 34 msimu huu wa majira ya joto.(***Express***)

**N'GOLO KUPEWA MKATABA**

CHELSEA wako tayari kumpatia mkataba mpya wenye donge nono kiungo wa kati wa Ufaransa, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 30. (***Fabrizio Romano, via Mail***)

**TORREIRA CHAMBO YA CORREA**

LAZIO wako tayari kumuuza mshambuliaji wa Argentina, Joaquin Correa mwenye umri wa miaka 26, ambaye ananyatiwa na Arsenal na Tottenham. Kuna uwezekano 'Washikabunduki' hao wakamtumia kiungo wa kati, Lucas Torreira mwenye umri wa miaka 25, kama sehemu ya mkataba. (***Gazzetta dello Sport***)

**CALHANOGLU APEWA MUDA**

KIUNGO wa kati wa Uturuki mwenye umri wa miaka 27, Hakan Calhanoglu, ambaye mkataba wake na AC Milan unamalizika msimu huu, amepewa muda wa mwisho kuamua hatima yake ya baadaye licha ya tetesi kwamba Arsenal wanamtaka. (***Express***)

**CENGIZ ATAKIWA FRANKFURT**

KLABU ya Eintracht Frankfurt wanamtaka winga wa AS Roma na Uturuki, Cengiz mwenye umri wa miaka 23, ambaye msimu uliopita alikuwa Leicester City kwa mkopo na huenda akauzwa kwa Euro milioni 10. (***Calciomercato***)

**BROM WAMTAKA CLUCAS**

KLABU ya West Brom imeonyesha nia ya kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Stoke City, Sam Clucas mwenye umri wa miaka 30. (***Football Insider***)

**ISMAEL ATAJWA BROM**

WEST Brom pia wanatarajiwa kumteua Valerien Ismael kuwa kocha wao mkuu baada ya kufikia kanuni ya makubaliano na Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 45. Ismael kwa sasa ni kocha wa Barnsley. (***Football Insider***)

**NEWCASTLE YAMTAKA WILLOCK**

NEWCASTLE inatafakari uwezekano wa kuipa Arsenal ofa ya mchezaji na fedha juu yake katika mkataba ambao utamwezesha kiungo wa kati, Joe Willock mwenye umri wa miaka 21, kurejea baada ya kukamilisha mkataba wake wa mkopo msimu uliopita. (***Express***)



# MWAMNYETO ATOA SABABU MWADUI KUIHENYESHA YANGA

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, amesema ushindi wa tabu walioupata dhidi ya Mwadui FC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara juzi, ni kutokana na awali kuidharau timu hiyo na kujiamini kupita kiasi kitu ambacho baadaye kiliwaponza na kufanya mchezo huo kuwa mgumu kwao.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa na Yanga kushinda mabao 3-2 dakika za mwisho kabisa, beki huyo wa kati aliyefunga moja ya mabao hayo, alisema ni kweli walijiamini kupita kiasi, lakini wakikosa mabao mengi hasa kipindi cha kwanza.

"Mechi ilikuwa ngumu kweli kweli, tunashukuru kwa kupata pointi tatu, tuseme tulijiamini kupita kiasi na tulikosa mabao ya wazi kipindi cha kwanza, ndiyo maana kipindi cha pili ikawa ngumu sana," alisema Mwamnyeto.

Kwa upande wa Mwadui FC, nahodha wa timu hiyo Jackson Shija, alisema walifanya makosa madogo mwishoni mwa mchezo yaliyowagharimu.

"Kwanza niipongeze Yanga, wamepambana hadi dakika za mwisho na kuweza kupata mabao mawili mwishoni. Sisi tulishindwa kuzuia, makosa madogo ndiyo yamesababisha watuadhibu," alisema.

Mchezaji huyo alishangazwa na watu wanaodai kwa nini walijituma sana kwenye mechi hiyo, akidai ulikuwa ni mchezo uliowaweka sokoni.

"Inashuka timu siyo wachezaji, mechi hii inaangaliwa sana, ndiyo maana kila mtu akaitolea macho. Kila mtu alitaka aonekane ili asindelee kukaa Mwadui, na kweli, mechi hii na zingine zilizobaki tutapambana ili tupate timu zingine za kutusajili," alisema.

Kwa matokeo hayo, Yanga imefikisha jumla ya pointi 67 ikiwa kwenye nafasi ya pili baada ya michezo 31, huku Mwadui ikiwa na pointi zake 19 na tayari ikiwa imeshashuka daraja.

**MILIKI...**



Mchezaji wa KMC FC, Cliff Buyoya (kushoto), akimiliki mpira huku Issa Rashid wa Mtibwa Sugar akihaha kumdhibiti katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kampeni ugombea urais ZFF sasa zapamba moto

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KAMATI ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), imefungua rasmi kampeni za kuelekea uchaguzi wa Rais wa Shirikisho hilo unaotarajiwa kufanyika Jumapili wiki hii visiwani hapa.

Uchaguzi huo unafanyika kutokana na kujiuzulu kwa aliyekuwa Rais wa shirikisho hilo, Seif Kombo Pandu mapema mwezi Februari mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili, Katibu wa Kamati ya Uchaguzi ya ZFF, Makungu Omar Makungu, alisema kampeni hizo zimefunguliwa tangu juzi baada ya kutokuwapo kwa pingamizi yoyote kwa wagombea.

Alisema Juni 19, mwaka huu, ilikuwa siku ya mwisho ya kupokea pingamizi kutoka kwa wadau wa soka kwa wagombea wote watano wa wanafasi hiyo waliopitishwa, lakini hakukuwa na aliyejitokeza kuwapinga.

"Tunashukuru mazoezi yote kwa mujibu wa ratiba yamekwenda kama yalivyopangwa, hakukuwapo na changamoto kubwa, labda ingetuzuia kufanya kazi zetu. Changamoto zilizokuwapo ni za kawaida tu za kibinadamu, hivyo sasa hivi tunaelekea katika kampeni.

Aidha, aliwataka wagombea wote watano kufanya kampeni za kistaarabu na kunadi sera zao ambazo zitaleta maendeleo mapana ya soka la Zanzibar.

Hata hivyo, aliwataka wagombea hao kufuata sheria za uchaguzi katika kipindi hiki cha kampeni hadi hapo Juni 26, mwaka huu majira ya saa 6:00 usiku, ambayo ni siku ya mwisho ya kampeni hizo.

Wagombea ambao wamepitishwa katika uchaguzi huo na kuanza kampeni ni Abdulatif Ali, Suleiman Shaban Suleiman, Haji Shehe Hamad, Suleiman Mahmoud Jabir na Abdulkadir Mohamed Abdulkadir "Tash".

## Ambundo anukia Yanga, Kibu bado

**Na Adam Fungamwango**

HARAKATI za usajili kwa ajili ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao na mechi za kimataifa umeanza, huku klabu ya Yanga ikitajwa kuwa kwenye mazungumzo ya kiungo wa Dodoma Jiji, Dickson Ambundo.

Meneja wa mchezaji huyo, Babu Ally, amethibitisha kwamba wamekuwa na mazungumzo na klabu ya Yanga, ingawa bado hayajakamilika lakini yanaendelea vizuri.

"Tumekuwa na mazungumzo na timu mbalimbali ikiwamo hata timu yake ya Dodoma Jiji ili wambakishe, lakini Yanga ndiyo inaoonekana kumhitaji zaidi. Mpaka sasa hakuna kilichokamilika, na kwa sasa mchezaji bado ana mkataba na timu ambao utamalizika ligi ikiisha," alisema meneja huyo.

Ambundo, mchezaji wa Kitanzania ambaye alijiunga na timu hiyo akitokea Gor Mahia ya Kenya, anayecheza nafasi ya kiungo mshambuliaji na amekuwa kwenye kiwango kizuri msimu huu kiasi cha kuvutia makocha wengi, akiwamo kocha wa Simba, Didier Gomes.

Wakati Yanga ikihusishwa na mchezaji huyo, Mwenyekiti wa Mbeya City, Vicent Msolla amesema kuwa mchezaji Kibu Denis bado ana mkataba wa klabu hiyo, hivyo haendi popote bila utaratibu wa kueleweka.

## Kipa Mwadui na penalti ya Fiston

**Na Saada Akida**

KIPA wa Mwadui FC, Mussa Mbisa, amesema kilichomsaidia hadi kuweza kuucheza mkwaju wa penalti juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkaka dhidi ya Yanga, ni kutokana na kuwa makini kumsoma mpigaji wa tuta hilo, Fiston Abdulrazak.

Kipa huyo aliibuka shujaa kwa kucheza mkwaju wa penalti hiyo wakati Yanga ikishinda mabao 3-2 kwa tabu dakika za mwisho za mchezo.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mbisa alisema siri ya kuokoa penalti hiyo ni baada ya kuona ukaaji wa mchezaji huyo na kusoma jinsi anavyopiga, hivyo kuisaidia timu yake kumaliza dakika 90 kwa kutofungwa mabao mengi.

"Nimeumia sana kushindwa kuulinda ushindi wetu, nina imani haikuwa bahati kwetu, tunaenda kujipanga kwa ajili ya mechi zetu zijazo kwa ajili ya kutafuta pointi kila mechi," alisema Mbisa.

Michezo
Jumanne Juni 22, 2021
Nipashe



POGBA SASA KULIPWA ZAIDI LIGI KUU ENGLAND HABARI UK 22

NIMEREJEA...



Kiungo wa Simba, Clatous Chama (kushoto), akiwa mazoezini na beki wa timu hiyo, Pascal Wawa, baada ya kurejea juzi na kuungana na wachezaji wenzake, akitokea kwao Zambia kwenye msiba wa mkewe. **MPIGAPICHA WETU**

## NABI AONYA USAJILI YANGA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameuonya uongozi wa Yanga kuhakikisha katika dirisha hili la usajili unafuata mapendekezo yake ili kuwa na timu imara itakayoweza kutoa ushindani msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano mingine timu hiyo itakayoshiriki.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Nabi alisema uongozi wa Yanga unapaswa kutumia maskauti mahiri kwa ajili ya kuangalia wachezaji aliowapendekeza ili kutekeleza vema ripoti yake kuelekea msimu ujao.

"Nimewaambia viongozi kwamba kabla ya kuanza usajili wanatakiwa kuunda timu ya maskauti ambao watafanya kazi kwa kushirikiana na uongozi kufuatilia wachezaji niliowapendekeza kuimarisha timu kwa msimu ujao," alisema Nabi.

Alisema mbinu ya kutumia maskauti ni baada ya kutaka kufuta makosa yaliyojitokeza kwenye miaka ya hivi karibuni, kwa kuhakikisha msimu huu wanafanya vizuri kwa kuisuka Yanga ijayo kuwa imara.

"Katika mapendekezo ya usajili kwenye ripoti yangu, nimetaja nafasi tu za wachezaji wala sikutaja jina, nina imani yale yote nimewaambia viongozi watafanyia kazi kwa ajili ya kuimarisha timu na kuwa bora zaidi ya sasa," alisema kocha huyo.

# SIMBA, YANGA SC DIMBANI SEPTEMBA MICHUANO CAF

### Azam FC nayo ndani katika ratiba hiyo, mbio sasa zabaki nani amalize...

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Soka barani Afrika (CAF), limetoa ratiba mpya ya michuano yake ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho kwa msimu ujao wa 2021/22 huku likiweka wazi kuwa ni rasmi sasa Tanzania itaingiza timu nne kwenye michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani humu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyolifikia Shirikisho la Soka nchini (TFF) rasmi na kutolewa na Ofisa Habari wake, Cliford Ndimbo jana, Tanzania ni miongoni mwa timu 12 ambazo zitaingiza timu nne, mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika kwa msimu wa 2021/22.

Taarifa hiyo imeeleza kuwa hatua ya awali itachezwa kati ya Septemba 10-12 na mechi za marudiano zikichezwa Septemba 17-19, mwaka huu, huku hatua ya makundi ikichezwa kati ya Februari 11-13, mwakani.

"Nafasi hizo [nne] zimepatikana baada ya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zilizokusanya alama nyingi zaidi kwenye viwango vya CAF," ilieleza taarifa hiyo.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Kanuni za TFF, timu itakayotwaa ubingwa wa Ligi Kuu na itakayoshika nafasi ya pili ndizo zitakazoiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa wakati itakayomaliza nafasi ya tatu na ile itakayotwaa Kombe la FA, zikiiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Kutokana na msimamo wa Ligi Kuu ulivyo kwa sasa, tayari Simba, Yanga na Azam zimekata tiketi ya kushiriki michuano hiyo ya CAF kwani hakuna timu yenye uwezo wa kufikia pointi zao.

Simba ina nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa huo kwa mara ya nne mfululizo na kuiwakilisha Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa kutokana na kuwa na pointi 70 kileleni zilizotokana na mechi 28 huku Yanga ikiwa nafasi ya pili kwa alama zake 67 baada ya kushuka dimbani mara 31 sawa na Azam FC iliyopo nafasi ya tatu kwa kuvuna pointi 63.

Timu inayofuata ni Biashara United yenye pointi 46, ambayo hata ikishinda mechi zake zote tatu zilizosalia kabla ya msimu kumalizika itaishia kufikisha jumla ya pointi 55.

Lakini, Simba, Yanga na Azam FC, bado zina nafasi nyingine ya kukata tiketi ya kushiriki michuano hiyo ya CAF kupitia Kombe la FA, kutokana na kufuzu hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo.

Katika hatua hiyo ya nusu fainali ya Kombe la FA, Ijumaa Yanga itakutana na Biashara United katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora wakati Jumamosi Simba ikiwa na shughuli pevu dhidi ya Azam FC kwenye Dimba la Majimaji mjini Songea.

Hatua ya Tanzania kuwa miongoni mwa timu 12 zilizokidhi viwango hivyo vya CAF na kupata nafasi ya kuingiza timu nne, imetokana na Simba kuvuna pointi nyingi baada ya kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu wa 2020/22, hivyo kuiwezesha kufikisha pointi 27.5 mbele ya Senegal iliyopo nafasi ya 13 kwa pointi zake 15.

Katika msimu wa 2017/18 wakati Yanga ikishiriki Ligi ya Mabingwa Afrika iliishia kuvuna pointi moja tu, huku msimu wa 2019/20, Simba ikiingiza pointi tisa na msimu huu wa 2020/21 ikiongeza pointi zingine 15 wakati Namungo iliyokuwa ikiiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho na kufika hatua ya makundi nayo ikivuna pointi 2.5 na kufanya jumla kuu kwa Tanzania kuwa na pointi 27.5.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002